# MWINGILIANOMATINI KATIKA *UTENZI WA FUMO LIYONGO* NA TAMTHILIA YA *KIFO KISIMANI*

**NA**

**KILINGO IRENE GAKII**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2019**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo kikuu chochote kingine kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili

**KILINGO IRENE GAKII** **TAREHE**

**C50/80399/2015**

**(MTAHINIWA)**

Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

**PROF. K. W. WAMITILA** **TAREHE**

**DKT. HANAH MWALIWA** **TAREHE**

# TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa wazazi wangu; marehemu babangu mpendwa Itikai Kilingo. Ingawa aliniacha ningali mdogo, ninaamini angezionea fahari, hizi juhudi zangu. Mamangu Kaloki Itikai kwa kuniwekea msingi thabiti katika masomo yangu na ambao umekuwa ngazi ninayoitumia kukwea hadi kufika kiwango hiki. Pia, sitamsahau marehemu mnuna wangu Munene Kilingo ambaye, mpaka kifo chake, alistahabu kuona nikipaa katika ngazi za kielimu. Wapendwa mliolala, pumzikeni kwa amani.

# SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa hekima ya kuendeleza masomo yangu mpaka kiwango hiki. Shukrani za kipekee pia ni kwa wasimamizi wangu; Prof. K. W. Wamitila na Dkt. Hanah Mwaliwa walionielekeza vyema na kunisaidia kujipanga ili nikamilishe kazi hii kwa wakati uliotakikana. Nawashukuru pia wahadhiri wote walionifundisha tangu nilipojiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi mnamo mwaka wa 2015, na kuhakikisha kuwa ndoto yangu ya kupata shahada hii imetimia. Wahadhiri hawa ni: Prof. Iribemwangi, Prof. Mwendah Mbatiah, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Habwe John, Prof. Rayya Timammy, Prof. Mbuthia Evans, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Prisca Jerono na Mwalimu Leonard Sanja. Vilevile ninashukuru usimamizi wa Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kunipa nafasi ya kuendeleza masomo yangu katika chuo hiki.

Shukrani za dhati pia zimwendee mume wangu mpendwa, Laibuni Mungania kwa kuvumilia upweke nilipokuwa nikihudhuria masomo yangu. Aidha, ulikuwa mwepesi wa kutumwa katika shughuli zilizochangia kufanikisha masoma haya. Vilevile, nawashukuru watoto wangu; Mutabari na Mwende kwa kuvumilia kukosa mapenzi ya mama mlipoyahitaji. Sitamsahau mama Jedidah Gachoka kwa kutunza watoto wangu vizuri nilipokuwa nikisoma.

Hali kadhalika, nawashukuru wanafunzi wenzangu katika kundi la tisa kwa maelekezo na midahalo tuliyokuwa nayo kipindi chote cha masomo haya. Nyote mlikuwa wa manufaa kwangu. Shukrani za dhati zimwendee Elizabeth Makena kwa maelekezo yako ya kutia moyo. Mawaidha yako yalinifaa sana. Mungu akuzidishie maarifa.

Hatimaye, nawashukuru walimu na wafanyikazi wa Shule ya Upili ya Kamacabi wakiongozwa na Bw. Kabithi na Bw. Nyamu, kwa mazingira mazuri mlionipa katika kipindi hiki chote cha masomo yangu. Hata hivyo, singeweza kuwataja wote waliochangia katika kufanikisha masomo yangu katika ukurasa huu. Nawashukuru nyote na kuwahimiza muwe mwanga na kielelezo bora kwa wasomi wengine.

# IKISIRI

Matini huweza kuakisiana kwa namna moja ama nyingine. Sababu ni kwamba, waandishi hujihusisha na kukusanya na kupanga yaliyoko katika kazi za awali ili kuunda kazi zao. Kwa sababu hii, kazi itakayoundwa itakuwa na mshabaha fulani wa kazi nyingine ya awali. Matini za kifasihi zinaweza kuingiliana kimatini. Mwingiliano huu unaweza kubainika sio tu katika kazi za utanzu mmoja bali pia katika kazi za tanzu tofauti za kifasihi. Utafiti huu umelenga kuthibitisha kauli hii kwa kuchunguza mwingilianomatini katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na tamthilia ya *Kifo Kisimani*. Katika kuhakiki haya, tumetumia nadharia ya mwingilianomatini iliyoasisiwa na mwananadharia wa Kifaransa; Julia Kristeva. Kutokana na utafiti huu, imebainika kuwa, kuna kuna vipengele vya mwingilianomatini katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani.* Hali kadhalika, kazi hizi zimeonyesha kuingiliana katika viwango vya usimulizi, maudhui, dhamira, uhusika na pia mandhari. Aidha, athari za mwingilianomatini katika udhamirishaji na mtindo wa tamthilia ya *Kifo Kisimani* zilibainika. Utafiti huu umethibitisha kuwa kuna mwingilianomatini katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani*.

## YALIYOMO

**UNGAMO** ii

**TABARUKU** .......... iii

**SHUKRANI** .......... iv

**IKISIRI** .......... v

**SURA YA KWANZA**

**UTANGULIZI**

1.1 Usuli wa Mada .......... 1

1.2 Tatizo la Utafiti .......... 2

1.3 Maswali ya Utafiti .......... 3

1.4 Madhumuni ya Utafiti .......... 4

1.5 Sababu ya Kuchagua Mada .......... 4

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti .......... 5

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada .......... 6

1.8 Msingi wa Kinadharia .......... 11

1.9 Mbinu za Utafiti .......... 16

Hitimisho .......... 17

**SURA YA PILI**

**MWINGILIANOMATINI KATIKA FASIHI**

2.1 Utangulizi .......... 18

2.2 Mwingilianomatini na Utohozi .......... 18

2.3 Vipengele vya Mwingilianomatini katika Fasihi .......... 19

2.3.1 Maudhui na Dhamira .......... 19

2.3.2 Uhusika .......... 20

2.3.3 Mandhari .......... 24

2.3.4 Usimulizi .......... 26

2.3.5 Msuko au Ploti .......... 27

2.3.6 Vipengele Vingine vya Mwingilianomatini .......... 28

Hitimisho .......... 29

## SURA YA TATU

## MWINGILIANOMATINI KATI YA UTENZI WA FUMO LIYONGO NA KIFO KISIMAN

3.1 Utangulizi ........ 30
3.2 Mwingiliano wa Kimaudhui ........ 30
3.2.1 Uongozi Mbaya na Athari Zake ........ 31
3.2.2 Mwanamke kama Nguzo ya Kimwingilianomatini ........ 34
3.2.3 Tamaa ........ 35
3.2.4 Usaliti ........ 38
3.3 Mwingiliano wa Uhusika ........ 39
3.4 Mwingiliano katika Usawiri wa Mandhari ........ 45
3.4.1 Mandhari ya Kijiografia ........ 45
3.4.2 Mandhari ya Kihistoria ........ 47
3.5 Mwingiliano wa Kiusimulizi ........ 49
3.5.1 Mwingiliano wa Ploti katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* ........ 50
3.5.2 Mwingiliano katika matumizi ya nyimbo na ngoma ........ 51
Mahitimisho ........ 52

## SURA YA NNE

## ATHARI ZA MWINGILIANOMATINI KATIKA UDHAMIRISHAJI NA MTINDO WA TAMTHILIA YA *KIFO KISIMANI*

4.1 Utangulizi ........ 54
4.2 Dhamira na Mwingilianomatini ........ 54
4.3 Mwingilianomatini wa Kimtindo ........ 56
4.3.1 Motifu ya Tanzia ........ 56
4.3.2 Motifu ya Usaliti ........ 58
4.3.3 Uteuzi wa Msamiati ........ 58
4.3.4 Matumizi ya Jazanda ........ 61
4.3.5 Tathmini ........ 63
Hitimisho ........ 64

**SURA YA TANO**

**MATOKEO YA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

5.1 Utangulizi .......... 66
5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti .......... 66
Hitimisho .......... 69
Mapendekezo .......... 70
**MAREJELEO** .......... 71

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Fasihi ni dhana ambayo inafahamika na watu wengi kwa jumla. Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999:9), fasihi ni 'sanaa inayohusu binadamu kwa namna maalum na ya kipekee.' Kauli hii in ya kweli kwani banadamu tu ndiye ana uwezo wa kujihusisha na fasihi; yaani, ndiye kiumbe wa pekee anayekuwa na uwezo wa kuwasiliana na binadamu mwingine kupitia fasihi. Mawasiliano haya huwezekana kwa kutumia lugha. Maoni ya Wamitila (2008:2) yanawiana na mawazo haya ya wa Njogu na Chimerah anaposema kuwa, lugha inayotumika katika fasihi sio lugha tu, bali ni lugha ya kisanaa. Ili kutumia lugha hii ipasavyo, msanii wa fasihi anapaswa kuitambua hadhira lengwa ili kuamua atakavyoitumia lugha yake ili kuwasilisha ujumbe anaokusudia. Hivyo, kwa mujibu wa maelezo haya tunaweza kusema kuwa, fasihi ni sanaa inayotumia lugha kwa ubunifu kuwasilisha ujumbe kwa binadamu. Ujumbe, huu unaorejelewa hapa, kwa jumla, unahusu migogoro ya kila siku ya binadamu.

Kwa mujibu wa fasiri hii, fasihi huangazia masuala mbalimbali yanayoikumba jamii. Masuala haya yanaweza kuwa ya kiuchumi, kiteknolojia, uongozi, dini, mapenzi, ndoa, n.k. Mambo haya huathiri binadamu yeyote yule ingawa kwa namna tofauti kulingana na mazingira anamoishi mtu fulani. Hivyo, mara nyingi utapata waandishi, katika harakati za kushughulikia masuala yanayoziathiri jamii zao, wameshughulikia mambo yanayoonyesha mfanano wa kiwango fulani. Hali hii, ndiyo husababisha kazi tofauti zinazolandana kimaudhui au hata kifani.

Hakuna kazi ya kifasihi inayoweza kuangaliwa kivyake kwa vile, kazi ya fasihi huundwa kutokana na kazi nyingine zilizoitangulia kazi inayochunguzwa. Kwa misingi hii, mwandishi huwa na jukumu la kukusanya na kupanga upya yaliyo kwenye mfumo wa utamaduni wake ili kuliafikia lengo lake. Kwa hivyo, mtunzi wa fasihi lazima aitambue hadhira yake ili kuchagua lugha inayofaa kutumiwa. Hatuwezi kutenganisha lugha na jamii kwani jamii hutumia lugha katika masuala ya kila siku kama vile: biashara, uongozi, elimu, teknolojia miongoni mwa mengine. Masuala haya ndiyo hasa hushughulikiwa na wanafasihi. Waandishi wanaweza kutumia lugha tofauti kurejelea kitu kimoja. Hili ndilo lililoangaziwa na Ferdnard de Saussure kama dhana ya ishara. Mwanaisimu huyu aliigawa ishara hii kama kiashiria na kiashiriwa. Hivyo,

kiashiria kinaweza kuwa tofauti lakini kiashiriwa kikawa kilekile kutegemea hadhira inayolengwa. Hivyo, ili kufanikisha ujumbe wake, mwandishi hana budi kurejelea ishara ya awali ili kuiwasilisha ishara yake. Kwa kufanya hivi kazi inayoundwa itakuwa kama mwangwi wa kazi ya awali inayohusiana nayo, na hivyo, katika kuihakiki matini lengwa, urejelezi wa matini za awali zinazohusiana nayo huwa na manufaa kwa vile hurahisisha uelewa wa matini inayochunguzwa.

Matini moja inaweza kuhusiana na matini nyingine. Uchunguzi ambao unalenga kubainisha uhusiano wa aina hii ni mwingilianomatini. Tafiti za awali zimeonyesha kuegemea uchunguzi wa mwingiliano wa kimatini baina ya kazi za utanzu mmoja licha ya kuwa, sifa ya mwingilianomatini inaweza kujitokeza hata baina ya kazi za tanzu tofauti za fasihi. Utafiti wetu ulijihusisha na uchunguzi wa mwingilianomatini kati ya kazi zilizoko kwenye tanzu tofauti. Hivyo, *Utenzi wa Fumo Liyongo* na tamthlia ya *Kifo Kisimani*, ziliteuliwa kimaksudi ili kuhusishwa katika kufanikisha utafiti huu kwani ni kazi za tanzu tofauti za fasihi.

*Utenzi wa Fumo Liyongo* (1913), ni miongoni mwa tenzi maarufu za Kiswahili. Utafiti wetu unajishughulisha tu na jinsi matini hii (utenzi uliotajwa) inavyoingiliana na matini ya *Kifo Kisimani*. Kama tulivyosema hapo awali kwamba, utenzi huu ni maarufu, umeweza kufanyiwa uchunguzi na watafiti mbalimbali. Hata hivyo, haujaonyesha kutafitiwa kuzingatia mwelekeo unaolengwa na utafiti huu. Kwa vile utenzi huu ulitungwa takriban karne moja iliyopita, hapa tunarejelea simulio la Kijumwa, inabainika kuwa athari zake katika udhamirishaji na mtindo wa tamthlia teule zimedhihirika wazi. Uteuzi wa tamthilia ya *Kifo Kisimani*, kuhusishwa katika utafiti wetu, uliafikiwa kwa vile inadhihirisha mwingiliano wa kimatini na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Tulichunguza viwango vya usimulizi, maudhui, dhamira, uhusika na mandhari ili kubainisha mwingilianomatini kati ya kazi teule. Hali kadhalika, tulichunguza athari za utenzi teule kwa udhamirishaji na mtindo wa tamthilia husika.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Matini mbalimbali za kifasihi zinaweza kuingiliana kwa namna moja ama nyingine. Hali hii, ndiyo humwezesha mhakiki kuielewa zaidi kazi fulani kwa kuihusisha na kazi ya awali inayohusiana na matini inayochunguzwa. Uelewa huu hurahisishwa na sababu ya kuwa, masuala au dhana fulani zinazoangaziwa katika matini inayochunguzwa, zimekwisha shughulikiwa hapo

awali. Aidha, kama Wamitila (2002:136) anavyosema, ni vyema ieleweke kuwa, mtazamo wa umwingilianomatini haujikiti katika 'wizi wa kimatini', japo pia unaweza kuwa ni aina ya mwingilianomatini, bali hujikita kwenye dhana kuwa, ishara hupata maana kutokana na kuhusishwa na ishara nyingine ya awali inayohusiana nayo. Hivyo, inakuwa wazi kuwa, waandishi na wahakiki wa matini za kifasihi, wanafaa wawe na maarifa ya kazi fulani za awali ili ziweze kuwaelekeza katika kuzalisha matini lengwa zenye maana zitakazozifaidi hadhira zao.

Mwingiliano wa kimatini unaweza kutokea katika tanzu mbalimbali za kifasihi. Kwa mfano, kunaweza kuwa na mwingiliano wa kimatini kati ya riwaya na riwaya, tamthilia na tamthilia au hata kazi za tanzu tofauti kama vile riwaya na tamthilia, ushairi na tamthilia n.k. Kimsingi ni kuwa, kazi za awali huchangia uelewaji wa maana ya matini inayochunguzwa. Tafiti zilizotangulia zimeonyesha kujikita katika uchunguzi wa mwingilianomatini baina ya kazi za utanzu mmoja. Hii ni licha ya kuwa, sifa hii ya mwingilianomatini inaweza kujitokeza hata baina ya kazi za tanzu tofauti. Ni kwa misingi hii, utafiti huu ulipania kuchunguza mwingilianomatini katika tamthlia ya *Kifo Kisimani* na *Utenzi Wa Fumo Liyongo*. Ulidhamiria kuchunguza viwango vya maudhui, usimulizi, dhamira, uhusika na mandhari ili kubainisha jinsi mwingilianomatini unavyojitokeza na kuchangia katika uendelezaji na uwasilishaji wa maana ya tamthilia teule.

**1.3 Maswali ya Utafiti**

(i). Je, ni vipengele vipi vya kimwingilianomatini vinavyobainika kati ya *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani?*

(ii). Je, mwingiliano unaobainika unadhihirika kwa viwango gani vya maudhui, dhamira, uhusika, usimulizi, na pia mandhari?

(iii). Je, mwingilianomatini huo una athari gani katika udhamirishaji na mtindo wa tamthilia ya *Kifo Kisimani*?

## 1.4 Madhumuni ya Utafiti

(i). Kubainisha vipengele vya mwingilianomatini katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani.*

(ii). Kuchunguza jinsi kazi teule zinavyoingiliana katika viwango vya usimulizi, maudhui, dhamira, uhusika na pia mandhari.

(iii). Kubainisha athari za mwingilianomatini katika udhamirishaji na mtindo wa tamthilia ya *Kifo Kisimani*.

## 1.5 Sababu ya Kuchagua Mada

Katika uhakiki wa fasihi, hakuna matini inayoweza kuangaliwa kivyake kwa vile lazima kuwe na matini nyingine inayoingiliana nayo. Hii ni kwa sababu, mwandishi huiga ishara ya awali kutoka kwenye mfumo lugha. Vipengele vinavyoweza kutolewa kwenye mfumo wa lugha sio tu maneno, bali hata ploti, uhusika, namna ya usimulizi, vishazi na hata sentensi. Kwa sababu hii, matini inayochunguzwa itaonyesha mfanano wa aina fulani na matini fulani ya awali. Yaani, tunaweza kusema kuwa, matini za awali huwa na adhari ya kiwango fulani kwa matini za baadaye zinazohusiana nayo. Na hivyo, katika kuihakiki kazi husika, mhakiki anafaa kuilinganisha na matini ya awali inayolingana nayo. Tafiti za awali zinadhibitisha kauli hii. Hata hivyo, nyingi za tafiti hizi zimeonekana kuegemea mwingiliano wa kimatini katika kazi za utanzu mmoja kama vile riwaya au tamthlia pekee, huku kazi za tanzu tofauti zikionekana kutengwa na tafiti hizi. Utafiti huu, unalenga kuongeza maarifa kuhusu suala la mwingilianomatini katika fasihi kwa kuchunguza mwingilianomatini katika kazi za tanzu mbili tofauti ambazo ni *Utenzi wa Fumo Liyongo* na tamthilia ya *Kifo Kisimani*.

Ikizingatiwa kwamba kazi hizi mbili zimo kwenye tanzu tofauti za fasihi, inatarajiwa kwamba utafiti huu utachangia kuelewa kuwa, mwingiliano wa kimatini unaweza kutokea popote pale katika kazi za kifasihi na wala sio katika kazi za utanzu mmoja tu kama ianavyoonekana kudokezwa na tafiti za awali. Mwingilianomatini baina ya kazi za tanzu tofauti ni uwanja ambao haujaonekana kushughulikiwa kwa kina na watafiti wa awali, ilhali kazi hizi zina sifa ya mwingilianomatini. Hivyo basi, utafiti huu, unalenga kuziba pengo hili la kiuhakiki. Tamthilia ya *Kifo Kisimani* na *Utenzi wa Fumo Liyongo* zimeteuliwa kuhusishwa katika utafiti huu kwa vile iliaminika kuwa zitasaidia kuafikia malengo ya utafiti huu. Tumechunguza jinsi kazi hizi

zinavyoingiliana katika viwango vya usimulizi, maudhui dhamira, uhusika na pia mandhari. Kwa kufanya hivi tunabainisha athari za kimwingilianomatini katika mtindo wa tamthilia teule.

Tumechagua nadharia ya mwingilianomatini kwa sababu ni nadharia inayotuwezesha kuchunguza uhusiano uliopo baina ya matini mbili au zaidi vizuri. Hii ndio sababu kuu ya kuhusisha kazi mbili tofauti katika utafiti huu ili tuzichunguze kwa misingi ya maelekezo haya. Athari za utenzi unaohusika katika utafiti wetu, (kazi tangulizi) katika udhamirishaji na mtindo wa tamthilia teule zimedhihirika.

Bila shaka, utafiti huu unakuwa wa manufaa kwa vile unaongeza maarifa kuhusu suala la mwingilianomatini katika kazi za fasihi hasa katika kazi za tanzu tofauti za fasihi. Huu in mchango muhimu katika fasihi na hasa ya Kiswahili. Hali kadhalika, unachangia katika uelewa wa kina wa kazi husika kwa vile zinachanganuliwa kwa kina ili kupata data ya utafiti huu. Kwa kufanya hivi, uelewa wa kazi hizi umerahisishwa kwa wasomi wa sasa na wa baadaye.

### 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti unahusisha *Utenzi wa Fumo Liyongo* na tamthilia ya *Kifo Kisimani*. Kazi hizi ziliteuliwa kimaksudi, zilisomwa na kuchanganuliwa kwa misingi ya nadharia ya mwingilianomatini. Utafiti huu, ulichunguza jinsi kazi hizi zinavyoingiliana kimatini katika viwango vya usimulizi, maudhui, dhamira, uhusika na pia mandhari. Ingawa waandishi wa kazi teule wameandika kazi nyingine za kifasihi, utafiti huu ulijikita kwa kazi zilizotajwa kwa vile, zinahusika moja kwa moja na mada ya utafiti. Kwa hivyo, data iliyopatikana katika kazi hizi, ilichangia kufanikisha kuafikia malengo ya utafiti.

Kuna madai kwamba, *Utenzi wa Fumo Liyongo* umetokana na fasihi simulizi ya Waswahili kumhusu jagina Liyongo aliyedaiwa kuishi kati ya karne ya kumi na tatu na kumi na tano. Hata hivyo, utafiti huu haukujihusisha na kubaini ingawa madai haya ni ya kweli au la kwani, utafiti wetu ulichukulia *Utenzi wa Fumo Liyongo* kama matini ya kifasihi tu jinsi ilivyo tamthilia ya *Kifo Kisimani.* Aidha, utafiti huu haujihusishi na historia ya Liyongo wa Waswahili kwani, haijafafanuliwa katika utenzi. Hivyo, tunajikita tu kwa dhana kwamba, wahusika ni viumbe wa kubuni wanaotumika na mwandishi kufanikisha ujumbe wake. Kwa sababu hii, kiwango cha uhusika kilichochunguzwa hapa, ni kile cha wahusika wa kubuni.

**1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada**

Wasomi mbalimbali wamefanya tafiti kuhusu suala la mwingilianomatini baina ya kazi mbalimbali. Njoroge (2007) ameshughulikia mwingilianomatini katika fasihi ya Kiswahili ambapo amejikita kwa riwaya mbili ambazo ni *Tata za Asumini* (1990) na *Rosa Mistika* (1988) zao Said A. Mohammed na Euphrase Kezilahabi katika mtririko huo. Njoroge aliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini katika utafiti wake. Alihakiki jinsi riwaya hizi zinavyoingiliana na kutofautiana. Njoroge alichunguza vipengele kama vile: wahusika, mandhari, ploti na maudhui. Alibainisha kuwa, baadhi ya kazi za kifasihi huingiliana kimatini na pia huchangizana. Hali hii, huwezesha kueleweka vizuri kwa matini kwa vile maana huwekwa wazi. Kulingana naye, binadamu wote kote ulimwenguni aghalau huathiriwa na takriban masuala sawa hivyo, sio ajabu kwa waandishi tofauti kuandikia matukio hayo kwa njia zinazolandana. Utafiti huu ulitufaa katika kuchunguza jinsi masuala yaliyoiathiri jamii iliyolengwa na *Utenzi wa Fumo Liyongo* yalivyoiathiri jamii lengwa ya *Kifo Kisimani*. Tulifanya hivi ili kutathmini jinsi masuala haya yanavyoingiliana katika kazi hizi.

Ochoki (2005), ameshughulikia mwingilianomatini katika riwaya mbili za Kezilahabi; *Nagona* (1990), na *Mzingile* (1991). Ochoki alihakiki kazi hizi kwa kuzilinganisha na kuzitofautisha na kazi za awali za Kezilahabi. Alitumia nadharia ya mwingilianomatini kuhakiki jinsi riwaya hizi zinavyoingiliana kimatini na fasihi simulizi na fasihi andishi kama vile riwaya za *Pedro Paramo* na *Babu Alipofufuka*. Ochoki alitambua kuwa, riwaya hizi zina vipengele vya fasihi simulizi hasa suala la majagina. Mfano, kisa cha Kakulu katika *Mzingile* kina sifa kadha zinazoweza kufananishwa na zile za visa vya fasihi simulizi hasa mighani. Hali kadhalika, mtafiti huyu anafafanua kuwa, kazi hizi, *Nagona* na *Mzingile*, zinaingiliana kimatini na fasihi andishi kama vile: riwaya ya *Pedro Paramo*, *Babu Alipofufuka*. Hapa, Ochoki alibainisha kuwa katika *Nagona*, *Mzingile* na *Pedro Paramo*, waandishi wametumia sitiari ya safari kuonyesha juhudi za binadamu katika kujitafuta na kuitafuta maana ya maisha yake. Aidha, katika kazi hizi alizozitafiti, binadamu amesawiriwa kama kiumbe kisichokuwa na uwezo wa kuudhibiti ulimwengu na kuufanya kumletea furaha. Kwa mfano, mhusika mkuu katika *Nagona* anafanya bidii kumtafuta Paa. Anapofanikiwa kumpata, huyu paa anampiga myeleka na kumwacha. Hali kadhalika, wahusika waliotumika katika kazi alizotafiti Ochoki, wamesawiriwa kwa njia isiyo ya kawaida. Mfano, kuna wahusika mizuka wanaofanya kazi kama watu walio hai. Kazi hizi

zinadhihirisha sifa ya umwingilianomatini kwa vile, zina vipengele vinavyoshabihiana. Hata hivyo, utafiti huu haukubainisha kama kuna mwingilianomatini baina ya *Nagona* na *Mzingile*. Katika utafiti huu, tulikusudia kubainisha mwingilianomatini baina ya kazi mbili za tanzu tofauti za fasihi. Tulilenga kutathmini jinsi matini hizi zinavyoingiliana katika vipengele vya maudhui na kifani. Hivyo, makala haya ya Ochoki yalitufaa kwa vile tuliyarejelea ili kubainisha vipengele vya kiuhakiki vinanavyoingiliana katika kazi teule.

Diegner (2005), ameangazia mwingilianomatini katika riwaya za Kiswahili, kwa kujikita katika riwaya ya *Nagona* (1990) yake Kezilahabi na *Ziraili na Zirani* (1999) ya William Mkufya. Hapa, Diegner alibaini kuwa, riwaya hizi mbili ni za kisasa. Kwamba, hazionyeshi kushughulikia tu masuala ya jamii ya Afrika Mashariki, bali masuala pana yanayohusu binadamu kwa jumla. Licha ya kuwa kazi hizi zimetungwa na waandishi tofauti na kipindi tofauti cha wakati, zinaonyesha kuingiliana kimaudhui. Hivyo, kazi hii imetufaa katika kubainisha mwingiliano wa kimaudhui. Kama inavyo shuhudiwa, hizi ni kazi za utanzu mmoja; riwaya, hata ingawa zinahusisha waandishi tofauti na kipindi tofauti cha utunzi wa kazi husika.

Ngesa na wengine (2015), wamechunguza mwingilianomatini katika tamthilia za Kiswahili, pale walihusisha tamthlia za *Mashetani* (1971) na *Kijiba cha Moyo* (2009) zao Hussein na Arege katika mtririko huo. Hapa, ilibainika kuwa, kutumika kwa tamthilia ya *Mashetani* kimwingilianomatini, kulifanikisha utunzi wa tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, na kwa njia moja ama nyingine, hali hii inachangia katika uchambuzi na uelewekaji wa tamthilia hizi mbili. Licha ya kuwa utafiti huu umehusisha kazi za utanzu mmoja, umetufaa kwa vile umetusaidia kuelewa zaidi dhana ya umwingilianomatini katika fasihi. Pia, utafiti huu umetusaidia kuelewa zaidi mchango wa *Utenzi wa Fumo Liyongo* katika uchambuzi na uelewekaji wa *Kifo Kisimani* hasa ikizingatiwa kuwa, kazi tunazozitafiti zimetengana kwa takriban kipindi cha karne moja. Kwa hali hii, tumechunguza jinsi utenzi huu unachangia katika uchambuzi na uelewekaji wa *Kifo Kisimani*.

Bosibori (2016), alichunguza mwingilianomatini katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (1834) yake Gogol na *Mstahiki Meya* (2009), yake Arege. Mtafiti huyu amechunguza vipengele vya ploti, wahusika, mandhari na maudhui. Alidhihirisha kuwa, kuna mwingiliano wa kifani na kimaudhui katika tamthilia hizi mbili alizohakiki. Aidha, Bosibori alitambua kwamba, waandishi waliokulia kwenye mazingira tofauti na vipindi vya wakati, wanaweza kuathiriwa na masuala sawa katika jamii wanamoishi na kuandika kazi zinazolandana kwa kiasi fulani. Hali hii inawezeshwa na ukweli kwamba, fasihi ni kioo cha jamii na kwa hivyo, huangazia mambo yanayoathiri jamii lengwa. Hivyo, athari za masuala haya, na zile za kazi za awali, alizowahi kuzisoma mwandishi, huwezesha kuzaliwa kwa kazi mpya inayofanana na kazi fulani ya awali. Kumaanisha kuwa, masuala yanayoathiri jamii ya sasa, yaliwahi kuiathiri jamii ya awali kwa namna moja au nyingine. Utafiti huu ulichangia katika kupata maarifa zaidi kuhusu masuala yanayoweza kuziathiri jamii mbalimbali ulimwenguni na kubainisha yale ambayo ni sawa kwa binadamu wote ambayo yanasababisha waandishi tofauti kuyashughulikia na hivyo kuibuka na kazi zinazolandana kwa kiwango fulani. Ikizingatiwa kuwa, kazi alizoshughulikia Bosibori zimetengana kwa kipindi kirefu sana cha wakati; zaidi ya karne moja, kazi hii imetufaa kwa vile utafiti wetu unahusisha pia kazi zilizotengana kwa kipindi kirefu cha wakati. Tunatathmini ni masuala yapi yanayoingiliana katika kazi zetu teule kama yanavyosawiriwa na waandishi hawa tofauti.

Kutokana na tathmini zilizotolewa hapo awali kuhusu tafiti zinazohusiana na suala la mwingilianomatini baina ya matini za kifasihi, imeonekana kuwa, tafiti hizi zinaelekea kujifunga kwenye kazi za utanzu mmoja tu wa kifasihi. Utafiti huu, ulinuia kuchukua mwelekeo tofauti kwa kuchunguza mwingiliano wa kimatini kati ya kazi za tanzu tofauti za fasihi. Hata hivyo, kazi hizi (zilizonukuliwa awali katika sehemu hii), zimetokea kuwa msingi mzuri wa kufanikisha utafiti wetu kwa vile, zimehusisha mwingiliano wa vipengele vya kifani na kimaudhui katika kazi zilizohakikiwa, vipengele ambayo vilevile vimetumika kubainisha hali ya mwingiliano wa kimatini katika utafiti huu. Kutokana na maelezo kuhusu tafiti za awali, inajitokeza kuwa, matini moja huwa ni mwangwi wa matini ya awali inayohusiana nayo. Yaani, ile matini ya awali inapata 'kuzaliwa upya' kupitia matini inayochunguzwa. Hii ni kwa sababu, matini ile ya awali huchangia msimbo fulani katika matini inayochunguzwa.

Ni kweli kwamba tafiti za awali zimeshughulikia suala la mwingilianomatini katika matini za fasihi. Hata hivyo, wataalamu hapa walionekana kuegemea kazi za utanzu mmoja, tofauti na inavyolengwa na utafiti huu ambao unahusisha kazi za tanzu tofauti. Pia, tamthilia ya *Kifo Kisimani* haijaonekana kuhakikiwa kwa mwelekeo unaochukuliwa na utafiti huu, licha ya kuwa na sifa ya umwingilianomatini na kazi nyingine. Hivyo basi, utafiti huu unadhamiria kuziba pengo hili la kitaaluma kwa kubainisha kwamba, mwingiliano wa kimatini huweza kutokea popote pale katika kazi za fasihi na wala sio katika kazi za utanzu mmoja pekee. Hali kadhalika, utafiti huu umebainisha jinsi mwingilianomatini unavyofanya kazi katika kazi za tanzu tofauti. Vilevile, mchango na athari za *Utenzi wa Fumo Liyongo* katika uendelezaji na ufanikishaji wa *Kifo Kisimani* umebainishwa.

Kuna tafiti nyingine ambazo zimefanywa na wataalam mbalimbali kuhusu kazi zilizoteuliwa kuhusishwa katika utafiti huu; Gathara (2015) alishughulikia taswira ya jagina katika tendi akijikita katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Utendi wa Nabii Isa*. Alitumia nadharia ya uhakiki wa vikale kulinganisha na kutofautisha sifa za mashujaa Liyongo na Isa. Hapa, Gathara alibaini kuwa, mashujaa hawa wana umuhimu mkubwa katika historia ya jamii zao na kwa ulimwengu mzima na kuwa wanaweza kuwekwa katika viwango sawa na mashujaa wengine ulimwenguni. Vilevile, alibaini kuwa sifa za mashujaa hawa, kwa kiasi kikubwa zinafanana. Licha ya kuwa utafiti huu umechukua mwelekeo tofauti kabisa na ule unaochukuliwa na utafiti wetu, makala haya yametufaa kwa vile tulihitaji sifa za mhusika Liyongo, ambaye ni mhusika mkuu katika utenzi teule, kubaini jinsi zinavyoingiliana na zile za Mwelusi, mhusika mkuu katika tamthilia teule. Kwa kufanya hivi, utafiti huu umetusaidia katika kuafikia lengo letu la tatu ambalo in kutathmini athari za *Utenzi wa Fumo Liyongo* katika mtindo wa tamthilia ya *Kifo Kisimani*.

King'ei (2001), alichunguza elementi za kihistoria katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Alibainisha kuwa, kuna elementi za kihistoria zinazopatikana katika utenzi huu. Ingawa utafiti wetu haujihusishi na historia ya mhusika Liyongo, iliyo nje ya utenzi teule, makala haya yalituwezesha kupata uelewa zaidi wa utenzi huu. Amefafanua historia ya *Utenzi wa Fumo Liyongo* katika makala haya. Ikizingatiwa kuwa uliandikwa karne kadha zilizopita, historia hii imetuwezesha kuelewa masuala kama vile, dhamira, maudhui na pia mandhari. Yametusaidia kuelewa hali ya jamii ambayo mwandishi wa utenzi huu alilenga kuwasiliana nayo, ili tubaini ni

kwa vipi baadhi ya masuala (maudhui) yaliyoiathiri jamii wakati huo yalivyokuwa yakiiathiri jamii ya wakati wa uandishi wa tamthilia ya *Kifo Kisimani*. Kwa kufanya hivi, tulibaini jinsi maudhui yanavyoingiliana katika kazi teule.

Waweru (2016), alitafiti usimilizi katika tamthilia za Wa Mberia. Tamthlia hizi ni: *Natala*, *Maua kwenye Jua la Asubuhi* na *Kifo Kisimani*. Alichunguza vipengele vya usimulizi kama vile: hadithi, nyimbo, sauti na methali. Alibainisha kuwa, usimulizi huchangia katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui katika kazi ya fasihi. Ni katika uchunguzi huu pia ambapo alitambua kuwa, Wa Mberia amefanikiwa katika kuichota, kuifinyanga na kubuni kisa kipya kuhusu mighani ya Fumo Liyongo iliyo na misingi yake katika fasihi simulizi ya waswahili. Kwa mujibu wa Waweru, ushujaa wa mhusika mkuu, Mwelusi, unaingiliana kwa kiasi kikubwa na ushujaa wa Fumo Liyongo. Ingawa makala haya yamejikita katika ulinganisho wa tamthilia husika na kisa cha fasihi simulizi, umehakiki kipengee cha usimulizi na hivyo umekuwa wa manufaa hasa katika kuhakiki vipengele vya usimulizi vya *Kifo Kisimani* vinavyoingiliana na vile vya *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

Kipyegon (2013), alichunguza nafasi na utambulisho wa mwanamke katika *Natala*, na *Kifo Kisimani*. Akimnukuu Mugambi (1982), Kipyegon anasema kuwa, fasihi in silaha mojawapo katika ghala ya silaha nyingi zinazotumiwa na tabaka moja kutetea maslahi yake katika mapambano. Kulingana naye, Mberia amefaulu kutumia silaha hii kupambana na unyanyasaji wa wanawake katika jamii. Anaendelea kusema kuwa, mwandishi huyu amefaulu vilivyo kumsawiri mwanamke katika jamii ya ki-ubabedume. Anaonyesha nafasi chukivu anayopewa mwanamke katika jamii ya aina hii. Licha ya hayo, mwandishi huyu anatoa mchango wake muhimu katika kumjenga mwanamke kihadhi. Hii ni kwa sababu, anampa mwanamke nafasi chanya na muhimu katika jamii. Kwa kifupi, mtafiti huyu aliangazia nafasi ya mwanamke katika jamii kama anavyosawiriwa na Wa Mberia. Licha ya haya, alichunguza changamoto za kijamii zinazochangia katika ukadamizaji wa wanawake.

Licha ya kuwa utafiti huu umechukua mwelekeo tofauti na utafiti wetu, tuliweza kuuurejelea tulipokuwa tunachanganua maudhui na uhusika hasa upande wa wanawake katika *Kifo Kisimani*. Bila shaka, kazi zetu teule zimehusisha wanawake. Ingawa sio kati ya wahusika wakuu, wametumiwa na waandishi hawa kufanikisha kazi zao kwa kuwapa nafasi muhimu katika kazi

hizi. Nafasi hizi zimechunguzwa kwa kina ili kutathmini jinsi usawiri wa mwanamke wa karne ya ishirini na moja katika *Kifo Kisimani* unavyoingiliana na usawiri wa mwanamke wa karne ya ishirini katika *Utenzi wa Fumo Liyongo.*

Kutokana na ufafanuzi huu, ni bayana kuwa, tafiti kadha zimefanywa zinazohusiana na mada yetu. Utafiti unaohusu nadharia ya mwingilianomatini umetuelekeza kubainisha ni vipi kazi zetu teule zinavyoingiliana hasa katika viwango vya maudhui, uhusika, usimulizi, dhamira na pia mandhari. Hali kadhalika, umetufaa katika uchunguzi wa athari za mwingilianomatini huu katika udhamirishaji na mtindo wa tamthilia husika. Kwa kufanya hivyo, tumeweza kubainisha mwingilianomatini uliopo baina ya kazi hizi teule. Hivyo, tunaweza kusema kuwa, nadharia hii inachangia kuafikia malengo ya utafiti huu na hivyo, kuufanikisha utafiti wenyewe.

Kwa upande mwingine, tafiti mbalimbali zinazohusu kazi tunazozishughulikia, zimekuwa za manufaa katika utafiti huu kwa vile zimehakiki vipengele mbalimbali tunavyovichunguza katika utafiti wetu. Hivyo, zimetupa ufafanuzi zaidi wa vipengele vyenyewe na kurahisha uelewa wake na hivyo, kutupa data ya kuaminika ya kuufanikisha utafiti wetu. Hali kadhalika, kutokana na uchunguzi wetu, tafiti za awali zilionekana kuegemea mwingilianomatini baina ya kazi za utanzu mmoja kama vile: riwaya na riwaya au hata tamthilia na tamthilia. Uchunguzi wa mwingilianomatini baina ya kazi za tanzu tofauti ulionekana kutoshughulikiwa kwa kina na kwa maoni yetu, kazi hizi pia zina sifa ya kimwingilianomatini. Hii ndiyo sababu tulichunguza mwingilianomatini baina ya kazi za tanzu mbili ambazo ni tamthilia na utenzi. Lengo la kufanya hivi, limekuwa kuliziba pengo hili la kiuhakiki.

## 1.8 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya mwingilianomatini. Allen (2000:35) anasema kuwa, kazi za kifasihi huundwa kutokana na kazi zilizotangulia. Kulingana naye, matini haina maana huru. Msomaji wa matini fulani hujiingiza kwenye mtandao wa mahusiano ya matini na hivyo, maana itakayopatikana, huwa ni kilichoko baina ya matini husika na matini nyingine yoyote ile inayohusiana na kuingiliana nayo. Hali hii, ndiyo Allen anayoita mwingilianomatini. Aidha, Allen anaendelea kusema kuwa, kazi yoyote ya sanaa haiwezi kuangaliwa kwa upekee na uhalisia wake kwa vile kazi hii iliundwa kutokana na kazi nyingine ya awali iliyohusiana nayo. Ni kwa sababu hii, utafiti wetu ulihusisha kazi mbili ili kuzihakiki kwa misingi ya maelezo haya.

Aidha Allen (2000:2-3) anaendelea kusema kuwa, nadharia hii imeonekana kupata misingi yake kutokana na nadharia za kiisimu na kifasihi zinazohusishwa na Ferdinand de Saussure na Bakhtin. Taaluma ya isimu iliangaziwa sana na mwanaisimu Ferdinand de Saussure ambapo aliangazia suala la ishara katika lugha. Saussure aliigawa ishara mara mbili; kiashiria na kiashiriwa. Kwa mujibu wa dhana hii, ishara hizi huwa za nasibu na hivyo, hupata maana yake kutokana na mifumo ya lugha na tamaduni zinamotumika. Hapa, Allen anafafanua kwamba, ishara hizi hupata maana yake kutokana na kuhusishwa na kuunganishwa na ishara nyingine. Hii ina maana kwamba, hakuna ishara iliyo na maana kivyake bali huhitaji kuhusishwa na ishara nyingine ili kupata maana inayokusudiwa. Nadharia ya mwingilianomatini inapata baadhi ya mizizi yake hapa kwa vile, hujihusisha na jinsi ishara hupata maana katika matini, baada ya kuihusisha na nyingine iliyoko kwenye matini ya awali.

Kwa upande mwingine, Bakhtin alijihusisha na jinsi semi au matini hupata maana yake kutokana na kuhusishwa na kazi zilizoitangulia. Bakhtin (1981), anasema kwamba, mtu hawezi kuuelewa usemi au hata kazi iliyoandikwa kama iliyo na maana ya kipekee kwa vile, semi au kazi hizi huhusishwa na kazi nyingine za awali. Aidha, anaendelea kusema kuwa, semi zote huwa ni jibu la semi na ruwaza za maana za awali. Kwa mujibu wa kauli hii, hakuna usemi au kazi iliyoandikwa iliyo na upekee wa maana kwa vile (kazi inayochunguzwa) huhusishwa na kazi nyingine za awali.

Bakhtin, hali kadhalika, alizungumzia dhana ya usemezano. Anasema kuwa, semi zote huwa ni za kiusemezano, na kwamba, maana ya semi hizi hutegemea semi za awali na jinsi zinavyopokelewa na hadhira lengwa. Anaongeza kuwa, neno lina pande mbili za kimatendo. Kwamba, maana yake inategemea tamko lenyewe limetolewa na nani, na linamwendea nani. Anaongeza kuwa, neno ni zao la uhusiano kati ya mzungumzaji na msikilizaji. Hivyo, kauli au maneno yatakayotumika katika mawasiliano fulani, yatategemea muktadha wa mazungumzo kama vile: wazungumzaji, mahali pa kuzungumzia, mada ya mazungumzo miongoni mwa masuala mengine, ili kuibua maana inayolengwa. Kwa mujibu wa Bakhtin, semi zinazotolewa huwa kwenye kategoria fulani ya usemi, na kwamba zina chembechembe za semi za awali. Kwa mujibu wa dhana hii, mwandishi wa matini ya kifasihi anapoanza kuandika, hujiingiza kwenye usemezano fulani na mwandishi aliyemtangulia. Kwa vile semi zote huwa ni za kiusemezano,

basi kila usemi huwa ni jibu la kitu kiingine na hivyo hutarajia kujibiwa. Hali hii, ndiyo Kristeva alikuja kuirejelea kama mwingilianomatini.

Kwa mujibu wa Allen, neno mwingilianomatini lilibuniwa na mwananadharia, Julia Kristeva miaka ya sitini. Allen anaeleza kwamba, Kristeva aliathiriwa na kazi ya Bakhtin hasa dhana ya usemezano. Katika nukuu, Allen anasema, "Kristeva alijishughulisha na kubainisha jinsi matini inavyoundwa kutokana na matini iliyotangulia. Kwa mujibu wa Kristeva, waandishi hawaundi kazi zao kutokana na akili zao asilia bali ni kutokana na kuunganisha mikusanyiko ya matini zilizotangulia. Kwa sababu hii, Kristeva anasema kwamba, matini ni mkusanyiko wa matini kadha zinazohusiana na kuingiliana kimatini, ambapo semi kadha, kutoka kwa matini nyingine, huingiliana na kukamilishana". Allen (2000:36-37). Maelezo haya ya Allen yametuelekeza kuchunguza athari za mwingilianomatini katika udhamirishaji na mtindo wa *Kifo Kisimani*. Kwa kufanya hivi, tuliweza kuafikia lengo letu la tatu la utafiti huu.

Raj (2015:77- 78), anaunga mkono maoni haya ya Allen kuhusu mwasisi wa nadharia hii ya mwingilianomatini. Aidha, anaongeza kuwa, nadharia hii inasisitiza kwamba, matini haiwezi kujitosheleza bila kuhusishwa na matini nyingine ya awali inayohusiana nayo. Kwa mujibu wa Raj, mwandishi huunda kazi yake kwa kusoma matini nyingine. Kuhusu dhana ya usemezano, Raj anafafanua kuwa, usemezano huu ni wa kibunifu ambapo maana hupangwa na wala sio kuumbwa. Hivyo, maana ya matini inayoundwa huwa maana pana kuliko ile inayopatikana kwenye matini yenyewe. Ni kwa sababu hii, tunatafsiri maana kwa misingi ya miktadha mbalimbali inayohusishwa nayo. Hali kadhalika, anafafanua kwamba, maoni ya Bakhtin ya usemezano yamejishughulisha na jinsi binadamu anavyotumia lugha katika miktadha tofauti ya kijamii, lakini Kristeva amejishughulisha zaidi na matini na umwingilianomatini. Hata hivyo, wote wanakubaliana kuwa, matini haiwezi kutenganishwa na misingi ya kijamii kwani ndiyo msingi ambapo matini huundwa. Maelekezo haya yametusaidia kubainisha maana za matini tunazozichunguza kwa kuzihusisha na miktadha mbalimbali. Kwa mfano, tunachunguza dhamira ya mwandishi wa *Kifo Kisimani* na ile ya *Utenzi wa Fumo Liyongo* ili kubainisha mwingiliano wake. Miktadha mbalimbali waliyoiandikia waandishi wa kazi hizi ndiyo imetuelekeza kubainisha dhamira za kazi zao.

Wamitila (2002:136) vile vile, ameangazia suala la mwingilianomatini. Kulingana naye, kazi ya fasihi haiwezi kujitegemea kwa vile lazima kuwe na matini nyingine ya awali inayohusiana nayo. Anaendelea kusema kuwa, tunapochunguza kazi za mwandishi mmoja, tunaona jinsi uashiriaji wa kazi za awali unavyosaidia katika uelewekaji wa kazi za baadaye. Mwingilianomatini huu, kwa mujibu wa Wamitila, sio wa urejelezi wa kazi fulani katika kazi nyingine tu, bali ni ule mwingiliano wa mitindo ya uashiriaji. Kwa mujibu wa Wamitila, mawazo haya ya Kristeva kuhusu mwingilianomatini yamewekewa msingi na mawazo ya Bakhtin hasa ile dhana ya usemezano. Bakhtin aliamini kwamba, mwandishi anapoanza kuiunda kazi yake hujiingiza kwenye usemezano wa aina fulani na mwandishi aliyemtangulia. Hivyo, kazi anayoiunda inakuwa kama mwangwi wa kazi ya awali inayohusiana nayo. Kwa mujibu wa Wamitila, matini huweza kuingiliana kwenye usawiri wahusika, uelezaji wa mandhari, matumizi ya mbinu za lugha n.k. Ni kwa misingi hii, tunachunguza jinsi *Kifo Kisimani* na *Utenzi wa Fumo Liyongo* zinavyoingiliana katika viwango vya maudhui, uhusika, usimulizi, dhamira na pia mandhari.

Nadharia hii huchukulia matini kama jira mbili; jira ya mlalo, ambayo huunganisha mwandishi na msomaji wa matini, na jira ya wima, ambayo huunganisha matini na matini nyingine. Mawasiliano kati ya mwandishi na msomaji wa matini huwezeshwa na uhusiano wa maneno ya matini husika na yale yaliyoitangulia matini hiyo. Mwandishi huzungumza na masomaji na wakati huo huo, matini 'huzungumza' kwa kuonyesha kuwepo kwa matini za awali zilizoko ndani yake. Hali hii inaonyesha jinsi jira hizi mbili zinavyofanya kazi katika matini na hali hii, kwa mujibu wa Allen, inasababisha kuzaliwa upya kwa nadharia ya usemezano yake Bakhtin, na ambayo inaishia kuwa mwingilianomatini. Kuhusu usemezano, Wamitila (2002:137), anaeleza kuwa, licha ya kuwa dhana hii ndiyo nguzo muhimu katika nadharia hii, baadhi ya wahakiki wanaochukua mkondo huu wameipanua nadharia ya mwingilianomatini kwa kutilia mkazo kwenye matini kuathiriana kuliko "sauti" kusemezana kama alivyokusudia Bakhtin.

Dhana zilizofafanuliwa awali zimeonyesha bayana kwamba, kazi za fasihi huundwa kutokana na kazi zilizotangulia na hivyo, hamna kazi inayoweza kuangaliwa kivyake bila kuhusishwa na nyingine ya awali inayohusiana nayo (kazi inayochunguzwa). Ni bayana pia kwamba, maana ya maneno ya mwandishi haitokani na upekee wake bali ni kwa mifumo ya lugha na utamaduni wake. Kwa mujibu wa nadharia hii, mwandishi huwa na jukumu la kukusanya ama kupanga

yaliyokuwemo katika mfumo wa lugha. Hivyo, kila neno, sentensi, aya au matini nzima atakayoiunda mwandishi, inapata asili na maana yake kutokana na mfumo wa lugha ambamo imeundiwa. Hali hii, inaeleza ni kwa nini kazi tofauti huonyesha mlandano wa aina fulani wakati wa usomaji na uhakiki wake.

Msingi huu wa nadharia ya mwingilianomatini ndio umetuwezesha kubainisha mwingilianomatini na maana kati ya *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* na athari za mwingilianomatini katika udhamirishaji na mtindo wa tamthilia teule. Kutokana na maelezo tuliyoyatoa hapa, tunaweza kuhitimisha sehemu hii kwa kutaja mihimili ifuatayo ya nadharia ya mwingilianomatini:

Kazi za fasihi huundwa kutokana na mifumo ya kanuni na tamaduni mbalimbali zilizowekwa na kazi tangulizi. Hii ni kwa sababu, kama baadhi ya wahaki wanavyoamini, hakuna matini inayojitosheleza bila kuhusishwa na matini nyingine ya awali inayohusiana nayo. Kwa hivyo, mwandishi anapoiunda kazi yake, hufanya hivyo kwa kusoma kazi nyingine. Na kwa sababu hii, kazi za awali huwekea kazi za baadaye misingi ya mifumo ya kanuni na tamaduni mbalimbali. Ni kwa misingi hii, tunahusisha kazi mbili katika utafiti huu ili tuhakiki athari za kazi ya awali (*Utenzi wa Fumo Liyongo*) kwa udhamirishaji wa kazi ya baadaye (*Kifo Kisimani*).

Maana ya maneno ya mwandishi haitokani na upekee wake bali ni kwa mifumo ya lugha na utamaduni wake. Hapa, mwandishi huwa na jukumu la kukusanya ama kupanga yaliyokuwemo katika mfumo wa lugha. Hivyo, maana ya matini atakayoiunda, itapata asili na maana yake kutokana na mfumo wa lugha ambamo imeundiwa. Mhimili huu unatuwezesha kuielewa miktadha mbalimbali iliyodhibiti uandishi wa kazi teule ili tubainishe maana mahususi ya kazi husika. Kwa kufanya hivi, tunaweza kuelewa dhamira ya waandishi wa kazi tunazozitafiti.

Matini yoyote huwa ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingi tangulizi. Hii ni kwa sababu, mwandishi hujihusisha na kukusanya na kupanga yaliyokuwemo hapo awali ili kuunda matini yake. Kwa hivyo, kauli inayonukuliwa hubadili na kueleza upya kauli asilia kwa kuiambatanisha na muktadha mwingine wa kiisimu na kijamii. Mhimili huu ulituwezesha kubainisha mchango wa *Utenzi wa Fumo Liyongo* katika udhamirishaji wa *Kifo Kisimani*. Kwa misingi ya mhimili huu, mwandishi anaweza kuathiriwa na kazi nyingi wakati wa kuunda kazi yake. Hata hivyo,

utafiti wetu ulijikita tu na kubainisha ni vipi kazi hizi mbili zinavyoingiliana. Hatukujihusisha na kubainisha kazi nyingine ambazo zinaweza kuwa zilimwathiri mwandishi wa tamthilia ya *Kifo Kisimani*.

Hakuna kazi ya kifasihi inayoweza kuangaliwa kivyake kwa vile, kazi ya fasihi huundwa kutokana na kazi nyingine zilizoitangulia. Hii ina maana kuwa, kazi za kifasihi hazijitegemei kimaana. Matini hupata maana inapohusishwa na matini ya awali. Hii ndiyo sababu, tunahusisha kazi mbili katika utafiti huu ili tuzihakiki kwa mwongozo huu. Tunahakiki jinsi tamthilia ya *Kifo Kisimani* ilivyofaidi kutokana na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Tumebainisha ni vipi tamthilia hii inapata maana baada ya kuihusisha na utenzi huu ambao, kwa hali hii, ndio kazi tangulizi.

Matini za kifasihi huwa zimechota, kunukuu, kuigeuza, kuiga na kwa namna ya kubeza au kurejelea kwa njia moja au nyingine, matini nyingine. Tunapania kudhibitisha kauli hii kwa kuhakiki jinsi kazi teule zinavyoingiliana na athari ya mwingilianomatini katika uashiriaji wa tamthilia husika. Kwa kufanya hivi, tumeweza kubainisha ni kwa namna ipi ambayo tamthilia ya *Kifo Kisimani* imepata kuiga, au kuurejelea utenzi teule katika udhamirishaji na mtindo wake.

**1.9 Mbinu za Utafiti**

Kazi hizi, *Utenzi wa Fumo Liyongo* na tamthilia ya *Kifo Kisimani,* ziliteuliwa kimksudi ili kushirikishwa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu, iliaminika kuwa, data ya kuaminika ya kufanikisha utafiti huu ingepatikana katika kazi hizi kwa vile zinahusiana na mada ya utafiti huu kwa njia ya moja kwa moja. Kazi hizi zilisomwa kwa kina ili kutambua vipengele vinavyoingiliana na vilevile, kubainisha athari ya mwingiliano huu kwenye tamthilia teule.

Data, inayodhihirisha mwingilianomatini katika kazi teule, imechanganuliwa kwa misingi ya nadharia ya mwingilianomatini. Nadharia hii inasisitiza kuwa, hakuna kazi ya fasihi inayoweza kuangaliwa kivyake bila kuhusishwa na matini ya awali inayohusiana nayo. Hivyo, ilituongoza kuhakiki kazi hizi kwa misingi hii. Hatua hii imetusaidia katika kubainisha vipengele vinavyoingiliana katika kazi teule pamoja na kufafanua athari za mwingiliano huu wa kimatini katika udhamirishaji na mtindo wa tamthilia teule.

Utafiti ulifanyiwa maktabani. Baadhi ya maktaba zilizotembelewa na mtafiti kukusanya data ni: maktaba ya Chuo Kikuu cha Nairobi na vilevile Chuo Kikuu cha Kenyatta. Katika maktaba hizi,

kazi hizi mbili zilisomwa kwa kina ili kupata data iliyohitajika kudhihirisha mwingilianomatini katika *Kifo Kisimani* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Aidha, kazi nyingine zinazohusu mwingilianomatini baina ya kazi mbalimbali za kifasihi, kama vile tasnifu, vitabu na majarida ya watafiti mbalimbali, zilisomwa ili kufanikisha utafiti huu. Pia makala ya mtandao yanayohusiana na utafiti huu yalisomwa na kubainisha mchango wake katika utafiti wetu. Data iliyopatikana imechanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo, utoaji wa mifano na unukuzi wa mambo muhimu kwa mujibu wa mada ya utafiti.

**Hitimisho**

Katika sura hii, tumefafanua vipengele mbalimbali ambavyo ni vya kimsingi katika utafiti wowote ule. Tumeangazia tatizo la utafiti, maswali na malengo ya utafiti na sababu za kuchagua mada kwa njia ya kitaalamu kwa kuwa maelezo mwafaka kuhusu dhana hizi ni muhimu katika utafiti. Hii ina maana kuwa, maelezo kuhusu dhana hizi yasipojitokeza wazi, basi huenda mtafiti asiweze kupata mwelekeo unaofaa katika kuendeleza utafiti wake. Aidha, tumebainisha makala tangulizi yanayohusiana na mada ya utafiti wetu na ufaafu wake katika utaratibu wa utafiti huu. Suala la msingi wa kinadharia pia limejadiliwa kwa kina kwani ndio unatuelekeza kuafikia malengo ya utafiti huu. Utafiti unaongozwa na nadharia ya mwingilianomatini katika uchanganuzi wa data ya utafiti iliyopatikana. Hatimaye, tumedhihirisha upeo na mipaka ya utafiti huu na vilevile mbinu za utafiti. Sehemu hii ni muhimu kwa vile inaonyesha shughuli za mtafiti na hivyo kumsaidia kupanga kazi yake na kuokoa muda wa kufanya utafiti.

# SURA YA PILI

# MWINGILIANOMATINI KATIKA FASIHI

## 2.1 Utangulizi

Mwingilianomatini, kama Wamitila (2003:158) anavyosema, ni dhana inayotumiwa kuelezea kuwepo kwa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani ya kifasihi. Kama tulivyosema hapo awali katika sura ya kwanza, nadharia ya mwingilianomatini hushikilia kuwa, matini moja huweza kuingiliana na kuhusiana na matini nyingine ya awali. Kulingana na Wamitila, mwingiliano na uhusiano huu unaweza kutokea kwa kile kinachoweza kuitwa 'mwanda wa kimwingilianomatini'. Mwanda hapa, ukiwa na maana ya upana wa kimahusiko wa kazi ya fasihi. Upana huu, unaweza kuhusisha mandhari, dhamira, uhusika, msuko, maudhui, mtindo wa kisimulizi na vilevile taswira. Hata hivyo, ni bora ieleweke kuwa, sio lazima matini ziingiliane katika vipengele hivi vyote. Baadhi ya matini huingiliana katika kipengele kimoja na matini nyingine zikaingiliana katika vipengele zaidi ya kimoja.

Katika sura hii, tutafafanua vipengele vya mwingilianomatini katika fasihi kwa jumla. Tutatoa mifano kutoka kwa matini mbalimbali zikiwemo kazi tunazozitafiti, pale vinapojitokeza katika kazi hizi. Kwa kufanya hivi, tutabainisha vipengele vya mwingilianomatini vinavyojitokeza katika kazi husika. Maelezo yanayotolewa katika sura hii ni muhimu kwa vile yatarahisisha uelewa wa dhana hizi na hivyo, kuweka msingi bora wa kuhakikia kazi zetu teule kimwingilianomatini. Hata hivyo, tutaonyesha jinsi *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* zinavyoingiliana, katika viwango vya vipengele hivi, katika sura zinazofuata.

## 2.2 Mwingilianomatini na Utohozi

Hizi ni dhana ambazo hurejelea uhusiano wa kimatini ingawa kwa namna tofauti. Kwa mujibu wa Wamitila ( 2003: 336), utohozi wa fasihi ni kule kuchukua kazi iliyoko katika utanzu mmoja na kuiwasilisha katika utanzu mwingine. Kwa mfano, kuweka riwaya katika muundo wa filamu. Hivyo matini inayoundwa kutokana na utohozi huwa ni matini ileile ya asilia lakini katika muundo mwingine. Kwa upande mwingine mwingilianomatini huhusisha kurejelea vipengele fulani vya kazi ya awali katika kuunda matini mpya. Matini zilizo na uhusiano wa kimwingilianomatini huwa ni matini tofauti kwa vile zina vipengele fulani vinavyozitofautisha matini hizi. Hivyo, tunaweza kusema kuwa mwandishi aliyeunda matini kiutohozi anaweza

kuwa kimelea wa matini ya awali kwani hajahusika katika kuunda matini mpya ila amebadilisha tu muundo wa kazi ya awali. Kwa upande mwingine mwandishi anayeunda kazi yake kimwingilianomatini huwa sio kimelea kwani kazi hizi mbili huwa tofatuti ingawa huwa na vipengele fulani vinavyohusiana. Utafiti huu umejikita katika uhusiano wa kimwangilianomatini na wala sio wa utohozi. Sababu ni kwamba matini tulizozichunguza zina vipengele vinavyozitofautisha. Hata hivyo katika utafiti wetu tumejikita katika vipengele vinavyodhihirisha mwingilianomatini katika fasihi na hasa, kazi teule.

### 2.3 Vipengele vya Mwingilianomatini katika Fasihi

Kwa mujibu wa Allen (2000:10-11), hakuna ishara iliyo na maana kivyake. Ishara hizi hupata maana kutokana na kuhusishwa na ishara nyingine. Hii ina maana kuwa, ili kupata maana ya ishara fulani, hasa matini ya kifasihi, tunapaswa kuihusisha matini husika na matini nyingine iliyoitangulia. Waandishi wa kifasihi hawachagui tu maneno kutoka kwa mfumo lugha, bali pia huchagua ploti, masuala ya uhusika, namna ya usimulizi, vishazi na hata sentensi kutoka kwa kazi nyingine za awali. Hili lina maana kuwa, kazi itakayoundwa, itakuwa inaiakisi kazi nyingine kwa kiwango fulani. Hali hii ndiyo inayojulikana kama mwingilianomatini. Vifuatavyo ni baadhi ya vipengele vinavyoweza kudhihirisha mwingilianomatini baina ya matini tofauti:

#### 2.3.1 Maudhui na Dhamira

Maudhui ni mawazo makuu yanayojitokeza katika kazi ya kifasihi ambayo huchangia kukuza mada ya mwandishi wa kazi fulani. Msanii anapoitunga kazi yake, huwa na lengo la kuwasilisha ujumbe fulani kwa hadhira yake. Mara nyingi, ujumbe huu hudhamiria kukuza maadili mema katika jamii. Ujumbe unaojitokeza hutegemea jinsi mwandishi alivyotumia mbinu mbalimbali za fasihi wakati anapoiunda kazi yake. Mbinu za usawiri wa wahusika na uchoraji wa mandhari za majazi zinaathiri kwa kiasi kikubwa mwelemeo wa wasomaji wa kujaribu kubainisha ujumbe katika kazi ya fasihi. Ujumbe huu ndio tunaoita maudhui. Kulingana na Wamitila (2002:173), kazi fulani inaweza kuiakisi nyingine kimaudhui, yaani kwa kuiongelea dhamira au maudhui yale yale. Mfano, maudhui katika 'Utenzi wa Hati' na *Utenzi wa Mwana Kupona* yanaonyesha mshabaha na hivyo, tunaweza kusema kuwa, kazi hizi zina sifa ya mwingilianomatini. Aidha, *Kifo Kisimani* na *Utenzi wa Fumo Liyongo* ni miongoni mwa kazi nyingine zinazoonyesha sifa

hii ya mwingilianomatini, pale ambapo zinaonyesha mwingiliano wa kimaudhui, kidhamira na katika vipengele vya fani.

Kwa upande mwingine, dhamira ni wazo kuu katika kazi ya fasihi. Wazo hili, hasa huhusiana na lengo la mwandishi wa kazi hiyo. Kwa mujibu wa Wamitila (2008:522), dhamira hukuzwa kwa njia mbalimbali kama vile: matumizi ya anwani ya kitabu, msuko pamoja na mahusiano ya wahusika mbalimbali katika kazi husika. Dhamira inahusiana na maudhui hivi kwamba, mwandishi anapokuza maudhui fulani, dhamira vilevile huweza kukuzwa. Kwa mfano, waandishi wa *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani*, wana dhamiria ya ukombozi. Ili kuafikia lengo hili, waandishi hawa wanaibua maudhui kama vile uongozi mbaya na athari zake. Athari za uongozi mbaya zinazojitokeza katika kazi hizi ni pamoja na; mauaji ya wanaodhaniwa kuwa wapinzani wa walio uongozini na ukosefu wa huduma bora kwa wananchi. Wapinzani wa uongozi wanapojaribu kipigana na suala hili, wanaafikia ukombozi ambao ndio lengo kuu la waandishi. Hili lina maana kuwa, mwandishi anapokuza maudhui ya uongozi mbaya, dhamira ya ukombozi inakuzwa pia. Hivyo, dhamira inahusiana na maudhui kwa kiwango kikubwa na vipengele hivi pia vinaweza kudhihirisha sifa ya mwingilianomatini katika matini mbalimbali.

### 2.3.2 Uhusika

Uhusika ni kipengele muhimu katika fasihi kwa vile hukuza maudhui na vilevile dhamira ya kazi husika. Hii ni kwa sababu, wahusika ndio nguzo au jira kuu ya matendo katika ulimwengu wa kibunilizi. Matendo yao ndio hutuelekeza kubainisha ujumbe wa mwandishi katika kazi husika. Uhusika huhusisha mbinu na mikakati inayotumika na waandishi katika usawiri wa wahusika katika kazi za kifasihi. Wahusika ni viumbe wa hadithini wanaotokana na wawazo ya mwandishi na wanaumbwa ili kuwasilisha ujumbe wa mwandishi (Njogu na Chimerah 1999:45). Ili kufanikisha ujumbe unaokusudiwa, baadhi ya waandishi huwasawiri wahusika walio na hulka na maingiliano wanayoyaona katika jamii ya hadhira lengwa. Hali hii huwezesha kazi za aina hii kuonyesha uhalisia wa maisha, ingawa nyingi huwa za kibunifu tu. Kwa mujibu wa Wamitila (2003:312), usawiri wa wahusika hurejelea jinsi wahusika wa kifasihi walivyochorwa au kuwasilishwa na msanii wa kazi husika. Usawiri huu unahusisha majina yao, lugha wanazopewa, majukumu yao ya kifasihi na kadhalika.

### 2.3.2.1 Mbinu za Kusawiri Wahusika

Sifa ya mwingilianomatini inaweza kujitokeza katika usawiri wa wahusika. Kazi zofauti huweza kuwa na wahusika walio na wasifu na tabia zinazolandana. Hili husababishwa na hali ambapo waandishi tofauti hutumia mbinu sawa za kusawiri wahusika katika kazi zao. Wahusika hawa wanapopewa wasifu unaofanana, mara nyingi, huchangia kuibua maudhui na dhamira zinazofanana na hivyo, kudhihirisha mwingilianomatini.

#### 23.2.1.1 Mbinu ya Kisimulizi

Hapa, mwandishi hutoa maelezo ya wasifu wa mhusika kiumbo na matendo yao. Waandishi wanaweza kutumia mbinu hii kimwingilianomatini. Kwa kawaida, sauti za wahusika ndio husikika sana katika tamthilia. Hii ni kwa sababu utanzu huu unahusisha mbinu ya mazungumzo sana kuliko masimulizi. Hata hivyo, sauti ya mwandishi inaweza kusikika hata ingawa ni kwa uchache. *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* zimeonyesha matumizi ya mbinu hii ya usawiri wa wahusika ambayo inadhihirisha sifa ya mwingilianomatini.

Kwa mfano, katika beti za 179, na 180 Kijumwa anatufafanulia wasifu wa Liyongo. Anatuambia kuwa, Liyongo alipodungwa tumboni, aliamka na kumfuata adui wake. Licha ya maumivu aliyokuwa nayo, mhusika huyu alikuwa na nguvu za kumfuata adui. Hii ni sifa ya ujagina kwa vile wao husawiriwa kuwa na nguvu zinazovuka mipaka ya ulimwengu halisi. Sifa hii inajitokeza katika *Kifo Kisimani* ukurasa wa 21. Mwandishi anatueleza ushujaa wa Mwelusi kuwa, licha ya maumivu aliyopitia baada ya kuchapwa na kuteswa na makachero kule gerezani, uso wake bado ulionyesha utulivu na ujasiri mkubwa. Hii ni kinyume na matarajio kuwa mtu mwenye maumivu huonyesha unyonge. Huu ni ujagina pia kama ilivyokuwa kwa mhusika Liyongo.

#### 2.3.2.1.2 Mbinu ya Kuwatumia Wahusika Wengine

Mwandishi pia anaweza kuwatumia wahusika kutoa maelezo kuhusu wahusika wenzao. Yaani, tunawajua kutokana na maneno yaliyotolewa na wahusika wengine. Licha ya kuwa kazi zetu teule zimo kwenye tanzu tofauti za kifasihi, mbinu hii imejitokeza katika kazi zote. Sauti za wahusika zimesikika katika utenzi teule ingawa ni ushairi ambapo tungetarajia sauti ya msimulizi kutawala. Hali hii inaonyesha mwingilianomatini kwa vile mbinu hii imetumika pia katika tamthilia teule. Mfano, katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* beti za 12 - 15, Mfalume anaeleza

sifa za mhusika Liyongo kuwa ni mwenye nguvu nyingi za kuwashinda watu mia kwa pamoja. Ushujaa wake unaonekana wazi katika beti hizi. Vilevile, mhusika Batu, katika *Kifo Kisimani*, anatueleza sifa ya mhusika Tanya kuwa ni mchezaji ngoma hodari. Mbinu hii inadhihirisha kuwa, mwingilianomatini unaweza kutokea hata baina ya kazi za tanzu tofauti zilizo na miundo tofauti.

**2.3.2.1.3 Mbinu ya Kidrama**

Kupitia mbinu hii, wahusika hujulikana kutokana na matendo au maneno yao wenyewe. Matendo na mazungumzo haya huibuka katika harakati za kuendeleza maudhui na dhamira ya mwandishi. Msomaji huweza kubainisha wasifu wa mhusika fulani kutokana na kile wanachokitekeleza katika kazi husika. Mfano, matendo ya Zakaria na Babake Asumini, katika *Rosa Mistika* na *Tata za Asumini* katika mtiririko huo, zinatuelekeza kubainisha sifa za wahusika hawa kama wenye taasubi ya kiume wanaoamini kuwa, nafasi ya mwanamke ni jikoni na kuwa mtiifu hasa kwa mwanamume. Hili linadhihirishwa na jinsi walivyowalinda watoto wao wa kike kwa madai kuwa wanawapa malezi mema. Hali kama hii pia inajitokeza kwa wahusika wawili katika riwaya za Ken Walibora. Mhusika Kongowea katika *Siku Njema* na Amani katika *Kidagaa Kimemwozea*. Matendo ya wahusika hawa yanatusawiria sifa zao kuwa ni wenye kupenda amani. Kongowea anapogundua kuwa Bi Rahma alikuwa na njama ya kumhini haki yake ya kumjua na kuwa mrithi wa mali ya babake, hakuwa na kinyongo naye. Alimsamehe na hakuwahi fikiria kulipiza kisasi. Vilevile, Amani alipogundua kuwa Majisifu alifanya maksudi ya kumhini haki yake ya kuwa mwandishi kwa kumwibia mswada wake na kuuchapisha kwa jina lake (Majisifu), hakuwa na kinyongo naye. Alimsamehe na akasonga mbele na maisha. Hata mhusika huyu (Amani) alipopata nafasi ya kulipiza kisasi dhidi ya Mtemi Nasaba Bora, aliyesababisha kifo cha babu yake na kunyakua ardhi hali iliyomwacha Amani katika umaskini mkubwa, hakufanya hivyo, hata alimwokoa mikononi mwa Gaddafi, aliyetaka kumuua (Nasaba Bora). Aidha, matendo ya Gege na mwana wa Liyongo katika *Kifo Kisimani* na *Utenzi wa Fumo Liyongo* katika mtririko huo, yanatuelekeza kubainisha kuwa wahusika hawa ni wenye tamaa na wanaweza kufanya chochote kile, hata mauaji, ili kupata wanachokitamani. Kile kitendo cha kuwaua wapendwa wao ili kupata mali, kinadhibitisha haya.

Matendo ya wahusika ni baadhi ya mambo yanayotuelekeza kubainisha maudhui na vilevile dhamira ya mwandishi. Matendo haya, kama tulivyobainisha hapo juu, yanaweza kudhihirisha

mwingilianomatini katika matini tofauti. *Kifo Kisimani* na *Utenzi wa Fumo Liyongo* zimeonyesha kutumia mbinu hii kimwingilianomatini na haya yatafafanuliwa kwa kina katika sura ya tatu.

**2.3.2.1.4 Mbinu ya Majazi**

Ni mbinu ambayo mwandishi humpa mhusika jina kulingana na tabia, sifa au matendo yake katika kazi ya fasihi. Mbinu hii, humrahisishia msomaji uelewa wa sifa za mhusika fulani kwa kulinganisha matendo au maneno yake na jina alilopewa. Wakati mwingine, majazi huhusisha matumizi ya kinaya au kejeli kutegemea ujumbe ambao mhusika huyo anapaswa kuwasilisha.

Mbinu hii imetumika kimwingilianomatini katika riwaya ya *Siku Njema* na *Kidagaa Kimemwozea*. Mhusika mkuu katika *Siku Njema* anajulikana kama Msanifu Kombo, ingawa alijulikana kwa lakabu ya Kongowea Mswahili. Jina Msanifu kombo ni la kimajazi kwa vile aliweza kubadili mtazamo wa wanajamii kuhusu watoto wanaozaliwa nje ya ndoa. Hali kadhalika, Kongowea alifunga safari ya kujisaka na mwishowe akafanikiwa kusanifisha yaliyokuwa yamemwendea kombo. Vilevile, mhusika mkuu katika *Kidagaa Kimemwozea* anajulikana kama Amani. Matendo yote yaliyotendwa na mhusika huyu yalikuwa ya amani. Hata alipogundua waliokuwa wamemnyima haki zake, alikabiliana nao kwa amani na mwishowe akapata ushindi. Hii ni mifano tu ya jinsi mbinu hii imetumika katika kazi hizi mbili. Usawiri huu wa wahusika unatusaidia kuelewa zaidi jinsi kazi hizi zinavyoakisiana na hivyo kuonyesha sifa ya mwingilianomatini. Hata hivyo, *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* hazijaonyesha matumizi ya mbinu hii. Hii pia ni ishara ya mwingilianomatini kwani kazi zote zimejitenga na mbinu hii.

**2.3.2.1.5 Mbinu ya Kimwingilianomatini**

Kwa mujibu wa Wamitila (2008:380), hii ni mbinu ya kusawiri wahusika hivi kwamba sifa zao zinalandana na za wahusika wa kazi nyingine za awali. Hata ingawa waandishi mara nyingine hubadilisha majina ya wahusika, sifa na matendo yao huweza kufanana kwa kiwango fulani. Sifa na matendo ya Mwelusi yanaingiliana na yale ya mhusika Liyongo. Alichukiwa sana na uongozi wa Bokono na hivyo, akapangiwa kuuawa. Alitiwa gerezani, akafaulu kutoroka lakini hatimaye aliuawa na kakake. Liyongo aliyapitia yaya haya, kwani hata naye aliishia kuuawa na mwanawe wa kiume. Tunaposoma *Kifo Kisimani* na kukutana na Mwelusi, tunamwona kama Liyongo

ingawa jina lake ni tofauti. Hali hii husaidia msomaji kuielewa zaidi tamthilia hii, hasa ikiwa amewahi kuusoma *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Hivyo, ni wazi kuwa mwingilianomatini huwezesha msomaji kuelewa kazi ya baadaye, anapoihusisha na na kazi ya awali inayohusiana nayo.

**2.3.2.1.6 Mbinu ya Kivisasili/Kitendi**

Mwandishi anaweza kusawiri mhusika aliye na sifa za kivisasili au kitendi. Wahusika wanaopatikana katika visasili au tendi hukiuka sifa za wahusika wa kawaida. Wahusika hawa hupewa uwezo wa kimatendo na kiakili na sifa zinazowakweza juu ya ulimwengu wao. Mbinu hii inaweza kutumika katika kazi nyingine za kifasihi mbali na visasili au tendi pekee. Kwa mujibu wa Wamitila (2008:381), mbinu hii inaweza kuangaliwa kama aina ya mwingilianomatini ikiwa mhusika anayezungumziwa anaweza kuhusishwa moja kwa moja na matini nyingine kama vile kisasili au utendi.

Kezilahabi, katika *Mzingile*, amemsawiri mhusika Kakulu kwa namna hii. Kakulu ameelezwa kama mhusika aliyekuwa na uwezo uliovuka mipaka ya matendo ya kawaida. Tunaelezwa kuwa mhusika huyu alizaliwa akiwa na nywele zilizochanganyika na mvi, alikata kitovu kwa meno yake, akajipangusa maji na kuwakaripia wanaume waliokuwa hapo karibu. Pia, baada ya kukua, alienda kuishi mlimani baada ya kuwafunza wazee watano kuhusu historia, mila na desturi. Sifa za mhusika huyu zinaingiliana na sifa za Yesu Masihi katika Biblia takatifu. Yesu anasemekana kuwa alizaliwa na bikira. Malaika ndiye aliyekuja kutangaza kuzaliwa kwake. Aidha, mhusika huyu alitenda mambo makuu kama vile: kukaa jangwani kwa muda wa siku arobaini bila kula chochote, kutembea juu ya maji bila kuzama, kufufua wafu, kutuliza dhoruba baharini na zaidi ya hayo, alipofariki, alifufuka na hadi leo Yesu anasemekana kuwa hai. Mbinu hii vilevile imetumika katika *Kifo Kisimani* ambapo Mwelusi amesawiriwa kama mhusika Liyongo katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Hata hivyo, haya yatajadiliwa kwa kina katika sura ya tatu.

**2.3.3 Mandhari**

Kulingana na Wamitila (2002:27-29), mandhari ni ile elementi katika kazi ya fasihi inayotufichulia wapi na lini ambapo matukio fulani yalifanyika. Hufafanua wakati na sehemu ambapo matukio ya msuko hutokea. Mandhari huwa muhimu hivi kwamba huweza kuathiri tabia za mhusika kwa kiasi kikubwa. Hii ni kwa sababu, mandhari huchangia katika kuwapa wahusika

wasifu fulani kutegemea mazingira anamojikuta kwayo. Pia mandhari huathiri sana mkondo wa kimaudhui na huwa na athari kubwa kwenye dhamira kuu katika kazi inayohusika. Mfano, katika mazingira ambamo mna viongozi dikteta wasiojali maslahi ya wanaoongoza, mwandishi anaweza kubuni mandhari yatakayooana na maudhui ya uongozi mbaya na athari zake ili kufanikisha dhamira yake. Vilevile, sifa za wahusika wanaokuza maudhui haya, lazima zioane na mandhari ya aina hii. Hii ndio sababu tunasema kuwa, mandhari huathiri sifa za wahusika, mkondo wa maudhui na vilevile dhamira.

Ingawa kuna aina kadha za mandhari, tumejikita katika aina mbili kuu za mandhari ambazo ni: mandhari ya kijiografia na mandhari ya kihistoria. Mandhari ya kijiografia hufafanua mahali maalum ambapo matukio ya kifasihi hutokea nayo mandhari ya kihistoria hujihusisha na kueleza kipindi cha wakati ambacho matukio ya kazi ya fasihi hutokea. Aina hii ya mandhari, huipa kazi husika msingi mzuri wa kihistoria na kiwakati. Hali hii humrahisishia msomaji uelewa wa kazi husika hasa katika masuala ya kihistoria.

Kwa mujibu wa Wamitila, mandhari huhusisha elementi tatu. Elementi hizi ni: Eneo halisi la kijiografia au maelezo ya jinsi chumba, sehemu au mahali fulani palivyo. Mathalani, mahali penye milima, mito, mwituni, bondeni, au hata kisimani. Vilevile, mandhari huhusisha amali za wahusika pamoja na namna na desturi za maisha yao ya kila siku. Hili hujumlisha mbinu mbalimbali za wanajamii za kuchuma mali (mfumo wa kiuchumi), mfumo wa kiutawala, imani, mahusiano na utangamano wao katika shughuli zao za kila siku. Mwisho, kuna elementi ya wakati ambapo tukio fulani linatendeka, awamu au kipindi maalum cha kihistoria au kipindi cha mwaka.

Kazi za fasihi zinaweza kuingiliana katika kipengele cha mandhari. Mfano, mandhari ya gereza imetumika katika *Kilio cha Haki* na *Kifo Kisimani*. Mandhari hii inatubainishia masaibu waliyoyapitia wapinzani wa utawala. Walidharauliwa na kuteswa na makachero ilhali hawakuwa na hatia yoyote. Vilevile, mandhari ya aina hii imetumika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* kwa sababu hii hii ya kuuzima upinzani. Waandishi wa kazi hizi walikuwa na dhamira ya ukombozi na mandhari hii inachangia katika kukuza dhamira hii. Katika utafiti huu, tumechunguza jinsi *Utenzi wa Fumo Liyongo* ulivyoingiliana kimandhari na tamthilia ya *Kifo Kisimani*. Mandhari

tuliyojadili ni kisimani, gerezani, ikuluni na vilevile vijijini. Haya yamejadiliwa kwa kina katika sura zinazofuata.

### 2.3.4 Usimulizi

Usimulizi ni uelezaji wa matukio katika hadithi. Usimulizi huu unaweza kuwa wa kubuni au ule unaotumia mbinu za fasihi simulizi. Katika utafiti wetu, tumejikita katika usimulizi unaotumia mbinu za fasihi simulizi. Kwa mujibu wa Wamitila (2002:44), waandishi wanaweza kutumia mbinu za kisimulizi zinazohusishwa na fasihi simulizi. Aidha, anaendelea kusema kuwa, sifa za fasihi simulizi zinajitokeza zaidi katika tamthilia au ushairi lakini pia huonekana katika riwaya. Mfano, katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, mshairi anasema anatunga hadithi ili vijana wajao wapate kuisikia.

*4. Hadithi niwandikiye*
*ya ajabu musikiye*
*yaliyojiri amriye*
*mupate kufahamiya.*

Hii ni mbinu ya fasihi simulizi kwani dhiyo inayoweza kusikizwa.

Kwa mujibu wa Waweru (2016:48), akiwanukuu Simpson (2004:20) na Cobrey (2005:1-5), usimulizi huhusisha vipengele viwili; kipengele cha ploti ambacho ni mpangilio wa matukio, yaani, tukio moja baada ya lingine katika hadithi. Kipengele cha pili ni kile cha usemi wa usimulizi ambao huhusisha vipengele vya kimtindo kama vile matumizi ya methali, kisengere nyuma, takriri na nyimbo na ngoma. Katika utafiti wetu, tumejikita na jinsi kazi zetu teule zinavyoingiliana katika vipengele vya ploti, nyimbo na ngoma.

Kama tutakavyoona katika sura ya tatu, usimulizi unaweza kuhusishwa na mwingilianomatini. Waandishi tofauti wanaweza kutumia mtindo sawa wa usimulizi. Kwa mfano, licha ya kuwa *Kifo Kisimani* na *Utenzi wa Fumo Liyongo* ni kazi za tanzu tofauti za kifasihi (ushairi na tamthilia), mitindo ya usimulizi inashabihiana. Sauti ya mwandishi inabainika katika tamthilia hasa pale anapotueleza wasifu wa mhusika fulani. Kwa mfano, anatupa umri wa mhusika ili kutusaidia kuwa na picha kamili ya mhusika huyu. Mwelusi anasemekana kuwa kijana wa kiume

mwenye umri wa miaka 24 hivi, naye Atega tunaambiwa kuwa ni msichana mwenye umri wa miaka 20 hivi. Aidha, Kijumwa anatueleza kuwa Liyongo alikuwa mwanamume mrefu na mpana. Utenzi unapoanza, Liyongo hakuwa ameoa, kumaanisha pia yeye alikuwa na sifa ya ujana kama ilivyokuwa kwa Mwelusi. Maelezo haya yanatusaidia kuelewa kuwa vijana wana nafasi muhimu katika kuleta mabadiliko katika jamii. Vilevile, sauti ya mhusika akieleza hulka ya mhusika mwenzake imetumika katika kazi zote mbili. Hatimaye, kazi hizi teule zimeonyesha kutumia ngoma na nyimbo kufanikisha maudhui na kukuza sifa za wahusika. Hali kadhalika, mfuatano wa matukio katika kazi zote mbili umedhihirisha mshabaha.

### 2.3.5 Msuko au Ploti

Kazi za kifasihi zinaweza kuingiliana kimsuko. Msuko, kwa mujibu wa Wamitila (2003:142), ni dhana inayorejelea mpangilio wa matukio yanayopatikana katika hadithi. Matukio haya hutegemea uhusiano wa kiusababishi. Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999:46), matukio ya kazi ya fasihi yanasababishana na kuelekezana kwenye usuluhisho fulani. Mpango wa matukio haya humwelekeza msomaji kuelewa dhamira ya mwandishi.

Ploti/msuko unaweza kuwa sahili au changamano. Katika msuko sahili, matukio huweza kufuatana moja kwa moja kutoka tukio la kwanza hadi la mwisho. Aina hii ya msuko pia huitwa msuko msago, na huwa umefuatana kwa mpangilio wa 'A-B-C-D' (Wamitila 2003:143). Msuko sahili ni rahisi kueleweka na msomaji ikilinganishwa na msuko changamano ambapo matukio hukatizwa na mbinu mbalimbali kama vile: mchezo ndani ya mchezo, mbinu rejeshi, kuwepo kwa msuko zaidi ya mmoja katika kazi moja ya fasihi na hali ambapo hadithi inaweza kuanza kwa maelezo yanayomalizia hadithi. Hali za aina hii, ndizo huleta uchangamano wa msuko katika kazi za kifasihi. Hata hivyo, kazi kuwa na ploti sahili, haimaanishi kuwa ni kazi dhaifu na vilevile, kazi iliyo na ploti changamano, haimaanishi kuwa ndiyo bora zaidi.

Matini zinaweza kuhusiana kimwingilianomatini katika kiwango cha msuko. Hali hii hutokea pale ambapo mfuatano wa matukio wa kazi fulani unaelekea kufanana na mfuatano wa matukio hayo katika kazi nyingine. Matukio yanaweza yakawa machache au mengi. *Tata za Asumini* na *Rosa Mistika* ni miongoni mwa kazi zinazoonyesha mwingilianomatinini katika kiwango cha msuko. Rosa na Asumini wamesawiriwa kama wasichana waliolelewa katika mizingira ya ubabe-dume. Baba zao waliwalinda kupita kiasi na kuwakataza mahusiano na wavulana kwani

waliona mahusiano ya aina hii ndio chanzo cha utovu wa maadili. Hatimaye, wasichana hawa wanapojiunga na vyuo, wanashindwa kuudhibiti uhuru wao mpya na kuishia kujiua. Aidha, msuko wa *Kifo Kisimani* unaingiliana na ule wa *Utenzi wa Fumo Liyongo* kwani, mengi ya aliyoyapitia Mwelusi, ni yale yaliyopitiwa na Liyongo. Hata hivyo, jambo hili litafafanuliwa kwa mapana katika sura zinazofuata.

### 2.3.6 Vipengele Vingine vya Mwingilianomatini

Mbali na vipengele tulivyovifafanua hapo awali, kuna njia nyingine zinazoweza kudhihirisha mwingilianomatini katika kazi ya fasihi. Njia hizi ni kama vile: unukuzi. Baadhi ya waandishi hunukuu sehemu za kazi za wengine katika kazi zao. Mfano, Matei katika *Chozi la Heri*, amenukuu moja kwa moja maneno yanayotoka kwenye Biblia takatifu. Katika ukurasa wa 47 anasema; "Tazama hii mikono yangu. Nipe mkono wako, utie ubavuni mwangu. Usikose kuamini tena. Amini." Mwandishi anasema maneno haya anapojaribu kueleza hali waliyokuwa wahusika Ridhaa na mwanawe Mwangeka walipokutana kwenye uwanja wa ndege baada ya kukumbwa na msiba wa kuwapoteza wapendwa wao. Maneno haya yamenukuliwa kutoka kwa Yohana 20:37, wakati Yesu alipojitokeza kwa wanafunzi wake baada ya kufufuka kwake. Mfuasi mmoja kwa jina Tomaso alikataa kuamini kabisa kwamba Yesu alikuwa amefufuka akisema mpaka aguse mkono na mbavu zake zilizodungwa kwa misumari. Sababu hii ndiyo iliyomfanya Yesu kumwambia amguse ili aweze kuamini. Vilevile, Kea katika *Kigogo*, ukurasa 65-66, amenukuu baadhi ya beti za wimbo wa Daudi Kabaka. Wimbo huu uliimbwa na mhusika Ngurumo akimrejelea Tunu. Ngurumo alikuwa akimkashifu Tunu ambaye alikuwa na shahada ya uzamifu katika sheria lakini alikuwa bado hajaolewa licha ya Majoka, kiongozi wa Sagamoyo, kumtaka aolewe na mwanawe. Hata hivyo, Tunu alikataa pendekezo hili la Majoka akisema huyo mtoto wa Majoka ni gumegume tu. Ukweli ma mambo ulikuwa kwamba, Tunu alikuwa mpinzani mkubwa wa Majoka na hii ndiyo iliyokuwa sababu kuu ya Ngurumo kumkejeli akitumia wimbo huu wa Kabaka; *Msichana wa Elimu*.

Mbinu hii ya unukuzi inaweza kujitokeza pia kama mbinu ya mhusianisho. Hii ni hali ambapo, msomaji anaposoma matini fulani, matini hiyo inamfanya akumbuke kazi ya awali inayohusiana na ile anayosoma. Hii ndiyo sababu tunaposoma maneno ya Matei, yaliyonukuliwa hapo juu, tunayahusisha na maneno ya Masihi Yesu Kristo katika Biblia takatifu. Vilevile, tunaposoma

kuhusu sifa, matendo na maisha ya Mwelusi katika *Kifo Kisimani*, yanatuelekeza kumhusisha na mhusika Liyongo wa *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

**Hitimisho**

Katika sura hii, tumejadili vipengele mbalimbali vya mwingilianomtini katika fasihi Tumejadili dhamira na maudhui na jinsi vipengele hivi vinaweza kudhihirisha mwingilianomatini katika kazi ya fasihi. Aidha, tumefafanua suala la wahusika na uhusika na mbinu mbalimbali zinazoweza kutumika na mwandishi kusawiri wahusika katika kazi yake ili kufanikisha lengo lake katika kazi hiyo. Hali kadhalika, tumeangalia mandhari kama kipengele cha mwingilianomatini. Tumefafanua umuhimu wa mandhari kwamba huweza kuathiri wasifu wa wahusika katika kazi ya fasihi. Isitoshe, tumeshughulikia suala la usimulizi na jinsi linaweza kujitokeza kama kipengele cha mwingilianomtini. Waandishi mbalimbali wanaweza kutumia vipengele sawa vya usimulizi katika kuwasilisha kazi zao. Hali hii inaweza kusababisha mlandano wa aina fulani na hivyo, mwingilianomatini ukajitokeza. Tumejadili pia suala la msuko na jinsi unavyoweza kubainisha hali ya mwingilianomatini. Matukio katika kazi tofauti yanaweza kupangwa kwa njia zinazofanana kwa kiwango fulani. Mbali na haya, tumejadili vipengele vya unukuzi na uhusianisho kama vipengele vya mwingilianomatini. Tumebainisha kuwa, mwandishi anaweza kunukuu maneno ya kazi nyingine ya awali na msomaji anapoyasoma, maneno yaliyonukuliwa, yanamwelekeza katika kukumbuka maneno aliyowahi kuyasoma awali na yanayohusiana na kazi ya sasa anayoisoma. Hata hivyo, katika sura hii, hatujajadili kwa mapana jinsi *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* zinavyoingiliana kimatini katika viwango vya vipengele tulivyovijadili katika sura hii. Ufafanuzi wa kina kuhusu suala hili umetolewa katika sura ya tatu na ya nne.

# SURA YA TATU

# MWINGILIANOMATINI KATI YA UTENZI WA FUMO LIYONGO NA KIFO KISIMANI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, tutajadili mwingilianomatini katika viwango vya kimaudhui na vipengele teule vya kifani katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na tamthilia ya *Kifo Kisimani*. Vipengele vya fani vitakavyozungumziwa ni: uhusika, mandhari na usimulizi. Tunadhamiria kubainisha jinsi wahusika walivyosawiriwa kimwingilianomatini ili kufanikisha dhamira na maudhui katika kazi husika. Vilevile, tutajadili suala la usimulizi ambapo tutajikita katika vipengele vya ploti na matumizi ya nyimbo na ngoma. Tutaeleza mwingilianomatini unaojitokeza katika vipengele hivi vya usimulizi. Hali kadhalika, tutabainisha jinsi mandhari yalivyosawiriwa na namna yanavyodhihirisha mwingilianomatini katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani*.

## 3.2 Mwingiliano wa Kimaudhui

Maudhui ni jumla ya mambo yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi. Mawazo haya huweza kudhibitiwa na mazingira anayoandikia mwandishi wa kazi husika. Mazingira huwaathiri waandishi kwa namna mbalimbali hivyo, tunaona waandishi tofauti wakiibuka na maudhui mbalimbali katika kazi zao ili kushughulikia masuala tofautitofauti yanayopatikana katika mazingira yao. Masuala haya, ni yale yanayoiathiri jamii ya mwandishi. Binadamu huathiriwa na masuala takribani yaliyo sawa. Kwa sababu hii, tunaweza kuona waandishi tofauti wakishughulikia mambo yanayoakisiana, kwa namna moja ama nyingine, ingawa wamo kwenye mazingira tofauti. Kwa mujibu wa nadharia ya mwingilianomatini, hakuna matini ya kifasihi inaweza kujitegemea kimaana bila kuhusishwa na matini ya awali inayohusiana nayo. Hii ni kwa sababu, matini huiakisi matini nyingine kwa namna moja ama nyingine (Allen 2000:1).

Miongoni mwa namna ambazo matini huweza kuakisi matini nyingine ni usawiri wa maudhui na dhamira. Kwa sababu hii, tunaweza kuona waandishi tofauti wakishughulikia maudhui na dhamira sawa katika kazi zao. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* kuna dhamira ya ukombozi. Katika kazi hizi mbili, wahusika wakuu, Liyongo na Mwelusi, wanachukua nafasi kuu katika mgogoro wa kazi zenyewe. Wote wawili wanaweza kuangaliwa kama wahusika wanaokinzana na viongozi wa nchi zao - Mfalme wa Pate katika utenzi husika na

Mtemi Bokono - katika tamthilia husika. Suala la mwingiliano wa kidhamira litajadiliwa kwa kina katika sura ya nne. Katika sehemu hii, tutajadili mwingiliano wa kimaudhui katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani*.

### 3.2.1 Uongozi Mbaya na Athari Zake

Waandishi wa kazi teule wameshughulikia suala la uongozi mbaya na athari zake. Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, Mfalme alikuwa ndiye mwenye kusema na alilosema halingepingwa na yeyote. Alikuwa mwenye wivu na alichukia yoyote aliyeona kwamba angeleta upinzani kwake. Alitumia vyombo vya dola kwa manufaa yake mwenyewe. Kwa sababu hii, umma ukawa ndio unaathirika zaidi. Vilevile, katika *Kifo Kisimani*, Bokono, ambaye alikuwa kiongozi wa Butangi, alikuwa dikteta. Alilosema halingepingwa. Wafuasi wake walimsujudu na walitekeleza amri zake bila swali lolote. Alikuwa mwenye tamaa ya uongozi na hakuwa tayari kuuachilia kwa mwingine. Kupitia uongozi mbaya wa viongozi hawa wawili, tunapata athari zifuatazo katika jamii:

#### 3.2.1.1 Mauaji ya Kiholela

Wapinzani wa viongozi hawa wote walinyamazishwa kwa kuuawa. Kwa mfano Mfalme, katika utenzi teule, alipoona kwamba Liyongo angempokonya ufalme, alipanga na Wasanye na Wadahalo kwamba wakiweza kumuua Liyongo na wampelekee kichwa chake kama thibitisho la kifo chake, basi, angewalipa riale mia. Watu hawa walikubali na kupanga jinsi wangemuua Liyongo ingawa hawakufaulu. Mfalme hakufa moyo, aliwaendea Ma-Shaha waliokuwa mjini. Akapanga nao kwamba waandae sherehe ya ngoma na wamwalike Liyongo. Mfalme alikuwa na nia ya kumkamata mhusika huyu pindi tu afikapo kwenye ngoma. Liyongo alipofika, alikamatwa na askari na kufungwa kwa pingu na minyororo na kufungiwa gerezani. Hapo, alipangiwa kuwa angeuawa baaada ya siku tatu, ingawa tena mpango huu haukufaulu. Baada ya kuwaza sana, Mfalme aliamua kumtumia mwanawe Liyongo. Alimwahidi mambo mengi mazuri, ikiwemo kumwoza bintiye. Hatimaye, mpango huu ulifaulu na Liyongo akauawa na mwanawe.

Katika *Kifo Kisimani*, baada ya Bokono kuhisi kwamba Mwelusi alikuwa tisho kwa utawala wake, alipanga akamatwe na kufungiwa gerezani. Kwa ushauri wa Batu na wengine, walipanga wamuue, kile walichokiita 'kuondoa mwiba kwenye mguu wa Butangi'. Mpango wa kumuua Mwelusi akiwa gerezani haukufaulu kwa vile alifanikiwa kutoroka. Baada ya kutoroka, ndipo

wazo la kumtumia Gege likamjia Mweke. Gege alikuwa kakake Mwelusi naye Mweke alikuwa kachero katika utawala wa Mtemi Bokono. Gege aliahidiwa mambo mazuri iwapo angesaidia kuuchomoa mwiba huu. Miongoni mwa ahadi alizopewa ni kuozwa bintiye Mtemi. Mpango huu ulifaulu na Mwelusi akauawa na kakake.

#### 3.2.1.2 Utabaka

Katika jamii zote mbili (zinazopatikana katika kazi zetu teule), tunaona kuna matabaka mawili; lile la walionacho na la wasionacho. Tabaka la juu ni la kundi tawala na tabaka la chini ni la kundi linalotawaliwa na tabaka la juu. Tabaka la chini linasujudu lile la juu. Wako tayari kutenda lolote linalosemwa na viongozi. Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, tabaka la maskini limo vijijini na walitegemea maji ya kisima kukata kiu chao. Kisimani kulipokuwa hakwendeki kwa sababu ya Liyongo kupatikana huko akionekana tayari kwa mashambulizi, watu waliteseka kwa ukosefu wa maji. Vilevile, katika *Kifo Kisimani*, tabaka la chini liliishi vijijini na walitegemea maji ya Kisima cha Mkomani kukata kiu chao. Kisima hiki kilipopigwa marufuku na uongozi wa Mtemi Bokono, watu waliteseka sana kama Andua anavyotudhihirishia katika ukurasa wa 91 kuwa, mateso ndiyo hewa waliyoipumua Wanabutangi.

Vilevile, tabaka la chini lilionekana kutumiwa vibaya na uongozi. Mfano, Mfalme anamwahidi mwanawe Liyongo kuwa angemwoza bintiye iwapo angefanikiwa kumuua babake. Kijana huyu anashawishika kwa urahisi na anamuua babake ingawa aliambulia patupu kwa vile, kiongozi huyu hakutimiza ahadi yake. Katika *Kifo Kisimani*, vilevile, tunaona Gege akitumiwa kumuua Mwelusi ambaye alidhaniwa kuwa anaupinga utawala wa Mtemi Bokono. Gege alidanganywa kuwa angeozwa bintiye Bokono iwapo angeweza kumuua kakake, Mwelusi. Hata hivyo, kijana huyu pia aliambulia patupu kwani ahadi hii pia ilikuwa ya uongo. Hivyo, tabaka la juu linatumia walio katika tabaka la chini kutekeleza maovu dhidi ya wapinzani wa kisiasa. Hatua hii ilikuwa mbinu ya viongozi hawa ya kujidumisha mamlakani. Kwa sababu ya tamaa, watawaliwa wanatekeleza waliyoagizwa na watawala bila pingamizi.

Wale wa tabaka la chini walioonyesha kuzinduka na kujua haki zao, walichukuliwa kuwa maadui wa utawala na hivyo uongozi ulibuni njia za kipigana nao ili kuuzima upinzani huo. Mfano, Liyongo alipoendelea kupata umaarufu na kupendwa na wengi kutokana na ushujaa wake, Mfalme alimwonea wivu. Alihisi kuwa Liyongo angempokonya ufalme siku moja hivyo,

akapanga kimuua. Kwa upande mwingine, Mwelusi alipoona kuwa yeye na wenzake wanateseka kwa kunyimwa maji ya Kisima cha Mkomani, aliamua kujitokeza na kuupinga utawala dhalimu wa Mtemi. Hali hii ilimfanya pia kupata umaarufu miongoni mwa Wanabutangi na kupendwa na wengi. Hata hivyo, ukakamavu huu ulimgharimu maisha yake kwani, alifariki akiwa kwenye harakati za ukombozi.

Uongozi mbaya ndio ulisababisha watu kugawika katika matabaka ya aina hii. Haya huwa mapenzi ya tabaka la juu ili liendelee kunufaika kutokana na lile la chini. Kwa hivyo, viongozi hawa, wa kazi zote mbili, hawangetia juhudi zozote za kuimarisha viwango wa watu vya kiuchumi, kwani kwa kufanya hivi, uongozi wao wa kidhalimu haungeweza kufaulu.

#### 3.2.1.3 Matumizi Mabaya ya Vyombo vya Dola

Uongozi katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* umeonyesha kutumia askari kwa manufaa yao wenyewe. Askari walitumika kunyamazisha waliodhaniwa kuwa na uwezo wa kupindua uongozi. Viongozi katika kazi zetu teule, wameonekana kutumia askari kutekeleza mbinu za kujidumisha mamlakani.

Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, Mfalme alipohusisha Wasanye na Wadahalo katika mpango wa kumuua Liyongo wakashindwa, aliamua kutumia askari. Alipanga na Ma-Shaha kuwa waandae sherehe ya ngoma na wamwalike Liyongo. Kwa vile Liyongo alikuwa hodari sana kwa ngoma na pia aliipenda, bila shaka hangekosa kuja na hivyo, Mfalme alijua fika kuwa, huo ndio ulikuwa wakati mwafaka wa kumkamata. Alipofika ngomani, Mfalme alituma askari mia waliokuwa wamejihami kwa mishale na magongo kwenda kumkamata Liyongo. Baada ya kumkamata, alifungwa kwa pingu na minyororo na kufungiwa kwenye chumba kimoja gerezani. Askari waliwekwa mlangoni kumlinda asitoroke. Walifanya kazi hii kwa zamu kuhakikisha kuwa Liyongo hapati mwanya wa kutoroka. Katika *Kifo Kisimani*, Mwelusi anakamatwa kwa kudaiwa kuwa kiongozi wa kundi haramu la Kabakaba. Kundi hili linadaiwa kuupinga uongozi wa Mtemi Bokono, jambo ambalo halikuruhusiwa Butangi. Alipokamatwa ili kuhojiwa na makachero kuhusu jambo hili la uchochezi, alipigwa na kuteswa sana ili akiri kosa hili. Alipokosa kutoa habari zozote, alifungwa kwa pingu na minyororo, akatiwa gerezani na kulindwa na askari watatu mlangoni. Askari hawa walilipwa kwa rasilimali za umma, lakini wakati huu, walifanya kazi iliyowahakikishia viongozi uongozi mrefu wa kidkteta. Badala ya askari hawa kulinda

wananchi kutokana na ukosefu wa usalama, wanawahangaisha watu wasio na hatia ili kuwafurahisha viongozi wao.

Katika visa hivi, tunaona kuwa viongozi katika kazi hizi mbili wametumia askari kwa manufaa yao. Viongozi hawa hawakutaka kuondoka uongozini na hivyo, walitumia mbinu zozote zile kujidumisha katika uongozi. Askari hawa nao walikuwa tayari kutekeleza amri ya kiongozi wao kwa vyovyote vile. Kiongozi anapaswa kutumia rasilimali za umma kwa manufaa ya umma. Anapotenda kinyume na hili, basi atakuwa ametumia mamlaka yake vibaya na vilevile, raslimali za umma. Vyombo vya dola vinapotumika kukidhi mahitaji ya kiongozi pekee na wala sio ya wananchi wote, basi vitakuwa vimetumika vibaya kama ilivyodhihirika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na tamthilia ya *Kifo Kisimani*.

### 3.2.2 Mwanamke kama Nguzo ya Kimwingilianomatini

Mwanamke amesawiriwa kama mhusika muhimu sana katika kazi zote mbili tulizozitafiti. Katika kazi hizi mbili (*Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani*), baba za wahusika wakuu hawakupewa nafasi yoyote. Babake Liyongo hatajwi na hivyo, hatuna habari zozote kumhusu. Kwa upande mwingine, tunajulishwa kuwa babake Mwelusi alikuwa amefariki na hivyo, hakupewa nafasi yoyote tamthiliani. Hali hizi zinawaacha kina mama wa mashujaa hawa na jukumu la kuwalea na kuwakuza hadi wakawa watu maarufu na mashujaa katika jamii zao tofauti. Kina mama hawa waliwapenda sana wanao. Liyongo na Mwelusi wanapotiwa gerezani, mama zao walikuwa wakipika chakula wapelekewe ingawa chakula hiki kiliishia kuliwa na askari waliolinda gereza.

Atega (katika *Kifo Kisimani)*, na mamake Liyongo (katika Utenzi wa Fumo Liyongo) walitumia uerevu wao kuwaokoa wapendwa wao kutoka gerezani. Wanawake hawa walitengeneza mkate wa wishwa na kuweka tupa ndani. Mkate wa wishwa, kwa mujibu wa kazi zote mbili, ulihusishwa na watu wenye hadhi ya chini katika jamii. Kwa sababu hii, askari katika kazi zote mbili waliudharau na kuwapelekea wafungwa; Liyongo na Mwelusi. Walipata tupa ndani na kuzitumia kukata minyororo waliyokuwa wamefungwa kwayo na hivyo, kujipatia uhuru. Ujanja uliofanywa na wanawake hawa umesawiriwa kimwingilianomatini kwani umetumika kutekeleza kazi sawa katika kazi zote mbili.

Aidha, wanawake wametumika kama mtego wa kuwanasa wanaume hasa wanapohitajika kutenda maovu. Alida, katika *Kifo Kisiman,i* na bintiye Mfalme katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* wametumika kuwanasa Gege na mwanawe Liyongo kwa mtiririko huo. Vijana hawa wa kiume waliahidiwa kuozwa mabinti hawa katika harusi ya kufana iwapo wangefanikiwa kuwaua jamaa zao. Jambo hili linaashiria kuwa, mwanamke hakuwa na usemi wowote hasa katika maamuzi yaliyofanywa na wanaume. Hatujaona, katika kazi zote mbili, mama za mabinti hawa wahusishwa katika uamuzi wa watakaowaoa wanao. Vilevile, wasichana wenyewe hajaulizwa maoni yao kuhusu jambo hili. Mzazi wa kiume akiamua jambo, ndilo huwa. Hii ndio sababu ilikuwa rahisi kwa vijana hawa kuamini ahadi walizopewa, kwani uamuzi wa aina hii haukuwa jambo geni katika jamii zao husika.

Kwa mujibu wa maelezo haya, ni bayana kuwa, kuna mwingilianomatini katika usawiri wa mwanamke kama nguzo ya kimwingilianomatini. Licha ya kuwa *Kifo Kisimani* iliandikwa mwanzo wa karne ya ishirini na moja, wakati mwanamke alikuwa ameshapevuka kimawazo na jamii ikaanza kuukubali upevu huu, bado tamthilia hii imesawiri mwanamke wa enzi za *Utenzi wa Fumo Liyongo* (1913), ambaye hakuwa amesoma na alikuwa akingoja maelekezo ya mwanamume ili kutekeleza jambo fulani. Mwanamke aliyeangaziwa na tamthilia hii ni yule wa kuzaa, kulea wana na kikaa jikoni akipikia familia yake kama ilivyo katika utenzi teule.

### 3.2.3 Tamaa

Hii ni hamu kubwa ya kupata kitu. Kichocheo cha maovu waliyoyatenda Mfalme na Bokono katika kazi hizi mbili, kilikuwa ni tamaa ya uongozi. Nukuu zifuatazo zinathibitisha hili:

*51. Na Sulutwani niseme*
*alikucha mwanamume*
*tampoka ufalume*
*dhana alimdhaniya.*

*91. Sulutwani kafikiri*
*"Kumuua ndio kheri*
*kumuwata ni khatari*

*kwa hila t'anizengeya*

*92. "Anipoke ufalume*

*kisa chanda nikiume*

*kheri yangu mwanamume*

*kumuua mara moya"*

Beti hizi zinadhihirisha kuwa mfalme alikuwa na wasiwasi kuwa Liyongo angempokonya uongozi hivyo, akaamua kumuua ili asije kujuta siku moja. Mauaji ya mhusika huyu yangehakikisha kuwa mfalme angeongoza kwa muda mrefu na bila hofu yoyote ya kuwa na mpinzani karibu naye. Vilevile, katika *Kifo Kisimani* tunaona Bokono akidhihirisha tamaa hii ya uongozi na kuishia kutekeleza mauaji.

*Nyalwe: Akili yangu ni timamu, timamu kabisa. [Akiiga sauti ya mumewe] Nitoeni!Nitoeni kaburini. Ondoeni udongo. Ondoeni udongo nitoke kaburini. Ondoeni Nitoeni kaburini! Nito-e-ni! Mnamzika mtu hai? Tamaa gani hii? Kunizika nikiwa hai, ili mchukue uongozi wangu!...*

(uk 14)

Mazungumzo haya yalikuwa baina ya Bokono na mkewe. Bibi yake alikuwa akirejelea ndoto aliyokuwa nayo Bokono usiku uliotangulia. Katika ndoto hii, Mtemi Bokono aliona watu wakijaribu kumzika akiwa hai ili wachukue uongozi wake. Ndoto hii ilimsumbua sana kiongozi huyu. Kutokana na mazungumzo haya, tunaelewa kuwa Bokono alikuwa na wasiwasi ya kupokonywa uongozi kwani alidhamiria kuongoza Butangi milele. Aidha, Bokono hakuwa tayari kupatiana uongozi kwa mtu mwingine ama kupokea upinzani wa aina yoyote kutoka kwa yeyote yule. Alikuwa tayari kufanya lolote ili kulinda nafasi yake ya uongozi. Mfano:

*Bokono: ... Siyo uongozi wangu! Kamwe siyo uongozi wa Mtemi Bokono! Niwaruhusu kuutia nyufa, abadani siyo mimi! Watakomeshwa. Watakomeshwa wakome kama walivyokoma kunyonya matiti ya mama zao! Uchochezi wao utakuwa mbio za sakafuni! [Kimya kifupi] Watakoma! Ah, mazuzu hawa! Wanamchezea mamba!...*

(uk 16)

Maneno haya ya Bokono yanadhihirisha tamaa ya uongozi aliyokuwa nayo. Kukomeshwa kwa "wachochezi" kunakorejelewa hapa ni mauaji ya wapinzani. Kupitia kuuawa, wahusika hawa wangenyamaza daima. Mifano tuliyoinukuu hapa inaonyesha wazi kuwa maovu waliyoyatenda Mfalme wa Pate, katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na Bokono, katika *Kifo Kisimani* yalichochewa na tamaa ya kuongoza jamii zao kwa kipindi kirefu. Tamaa hii iliwafanya kutekeleza mauaji ya waliodhaniwa kuwa wapinzani na washindani wao katika uongozi.

Hali kadhalika, wahusika Gege na mwana wa Liyongo wanadhihirisha tamaa katika kazi teule. Wawili hawa waliahidiwa kuozwa mabinti wa viongozi iwapo wangefanikiwa kuwaua Mwelusi na Liyongo kwa mtiririko huo. Kuozwa binti wa kiongozi wa nchi kuliandamana na mambo mengine mazuri kama vile kupata utajiri. Hili liliwatia tamaa vijana hawa na kuishia kutekeleza mauaji. Katika utenzi teule, mwana wa Liyongo aliingiwa na tamaa alipoambiwa na Mfalme jinsi angemwoza bintiye katika harusi ya kufana. Alifurahi sana na akaamini kuwa mfalme angemtendea hili. Tamaa hii inadhihirishwa na ubeti wa 156.

156. *Kijana kafurahika*
*tamaa zikamshika*
*"Nakuona hakika*
*huwa watanitendeya"*

Aidha, tamaa hii hii inajitokeza katika tamthilia teule, kama inavyodhihirishwa na sauti zinazomjia Gege akilini baada ya Mweke na Talui kumhadaa jinsi angeozwa Alida katika harusi ya kufana.

*Sauti I : Mfunge Mwelusi kinywa upate maisha mazuri.*

*Sauti II : La, Gege. Usimfunge nduguyo kinywa*

*Sauti I : Usikatae hurulaini kwa ajili ya kuogopa. Usiogope kashifa. Watu watasema na kuchoka.Usikatae mali na umaarufu kwa ajili ya kuogopa kunyoshewa vidole. Kunyoshewa vidole sio kufumwa kwa mishale. Ndiyo,Gege, ndoa na bintiye Mtemi ni lango la kuingia kwenye umaarufu Usikatae kukanyaga vidato vyake. Ndoa, Gege, ndoa, inakunyoshea mikono. Nyosha mikono yako uikaribishe! Karibisha maisha mapya, Gege!*

(uk 74)

Tamaa ya mali ndio iliyowafanya Gege na mwana wa Liyongo kuwaua jamaa zao. Hata hivyo, wote waliambulia patupu kwani ahadi hizi zote zilikuwa za uongo.

Vilevile, askari wamesawiriwa kama wahusika wenye tamaa ya chakula. Wao walipenda kula vyakula vya wafungwa vilivyoletwa na wapendwa wao. Mfano, Liyongo alipokuwa gerezani, mamake alikuwa akitayarisha chakula kizuri ili kipelekewe mwanawe. Chakula hiki hakikuwahi kumfikia kwani askari waliolinda gereza walikuwa wakila chote. Pia, chakula alichokuwa akipelekewa Mwelusi kule gerezani, hakikuwahi kumfikia kwa vile, askari walinda gereza pia walikula chote kilipofika mikononi mwao. Mkate wa wishwa unapoletwa kwa wafungwa hawa, askari wanaudharau kwa vile haukuwa mzuri. Hili lina maana kuwa, kungeletwa mkate wa aina nyingine nzuri, hata huo haungewafikia wafungwa hawa. Mkate huu 'mbaya' ndio uliowanusuru wafungwa hawa. Ulafi unawafanya askari kutowajibika katika kazi zao.

**3.2.4 Usaliti**

Mfalme alipojaribu mbinu kadha za kumuua Liyongo na kushindwa, aliamua kumtumia mwana wa Liyongo. Kijana huyu alipomwendea babake akitaka kujua kile kingeweza kumuua, Liyongo hakuona ugumu wowote kumwambia mwanawe siri hiyo. Kijana huyu alipopata habari hizi, alimwambia Mfalme ambaye alimwagiza kumuua babake mwenyewe. Hivyo basi, mwana wa Liyongo akamuua babake kwa kumdunga sindano ya shaba kwenye kitovu chake alipokuwa amelala. Huu ni usaliti kwa vile Liyongo alimwamini mwanawe na kumpa siri aliyoitumia kumwangamiza shujaa huyu.

Gege, alitumiwa na utawala wa Bokono kumuua Mwelusi katika *Kifo Kisimani*. Kakake alipotoroka gerezani, Gege alikuja kumtafuta nyumbani. Ingawa mama yao alikuwa amekataa kusema alikokuwa Mwelusi, Gege alijifanya kubadilisha mwelekeo wake kuhusu kakake na hili lilimshawishi Tanya kumpa siri ya alikokuwa Mwelusi. Alipopata habari hizi, Gege alimwandama hadi kisimani akijifanya kuwa na "habari muhimu" alizosema kuwa zilitoka kwa mama yao. Hili lilimfanya Mwelusi kumwamini na akakubali wakaenda chemba ambapo Gege alimdunga kisu tumboni na kumuua.

Mauaji haya yote yalitekelezwa na watu wa karibu sana na wahusika waliofariki. Wauaji hawa, walipaswa kuwa wasiri wao lakini wakabadilika na kuwa wasaliti na kuwaua watu waliopaswa

kuwalinda. Haya yote ni kwa sababu ya tamaa na umaarufu. Hali hii pia imejitokeza kimwingilianomatini. Waliofariki wameuawa kwa njia zinazofanana; kudungwa tumboni kwa vifaa vikali na waliotekeleza mauaji ni jamaa wa karibu sana wahasiriwa.

### 3.3 Mwingiliano wa Uhusika

Mwandishi wa matini fulani anapotaka kumsawiri mhusika mwenye wasifu fulani katika matini yake, kuna uwezekano akilini mwake, awe na mhusika mwenye wasifu huo huo anayepatikana katika matini nyingine ya awali (Allen 2000:12). Hii ina maana kwamba, mhusika huyu wa matini ya sasa atakuwa na wasifu unaofanana kwa kiwango fulani na yule wa matini iliyotangulia. Mwingiliano wa uhusika unaweza kutokea kwa namna mbalimbali. Kwanza, katika kuwepo kwa mfanano wa moja kwa moja wa majina. Kwa mfano, katika *Maumbile si Huja*, kuna mwanamke ambaye alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mfanyikazi wake. Mwanamke huyu alijulikana kama Amina. Vilevile, katika *Asali Chungu* kuna mwanamke mwenye sifa kama hizo za Amina ambaye pia alijulikana kama Amina. Hali kadhalika, wahusika wanaweza kuingiliana kwa kuwepo na uhamasishaji na utendaji sawa, msukumo unaofanana, kubainisha sifa zao. Kuna mwingilianomatini katika usawiri wa wahusika katika kazi zote mbili. Mwingilianomatini huu unajitokeza ifuatavyo:

#### Liyongo na Mwelusi

Wahusika hawa wamesawiriwa kwa njia zinazolandana. Katika mwanzo wa utenzi, Liyongo anaonekana kijana mwenye umbo zuri linaloashiria ushujaa. Katika jamii za Kiafrika, vijana ndio waliopewa jukumu la kupigania jamii zao dhidi ya maadui waliojitokeza kuchukua mifugo na mali nyingine ya thamani. Mwelusi, kwa upande mwingine, ni kijana wa kiume mwenye umri wa miaka 24 hivi. Huyu pia ni kijana anayeweza kuipigania jamii yake.

Wahusika hawa wote walikuwa maarufu sana na walipendwa na wanajamii. Umaarufu huu ndio uliowafanya viongozi katika jamii zao husika kuwaogopa kuwa wangewapokonya uongozi na hivyo, wanawapangia kuwaua. Hatimaye, wahusika hawa, ambao ni wahusika wakuu katika kazi zote mbili, wanauawa na jamaa zao kama ilivyokuwa imepangwa. Kifo chao pia kinatokea kimwingilianomatini ambapo wanasalitiwa na wendani wao. Liyongo anasalitiwa na mwanawe

naye Mwelusi anasalitiwa na kakake. Aidha, wahusika hawa walikufa kwa kudungwa tumboni na wote walifia kisimani.

Vilevile, Liyongo na Mwelusi ni waadilifu. Katika ubeti ufuatao, tunaambiwa:

*6. Liyongo kitakamali*
*akabalighi rijali*
*akawa mtu wa kweli*
*na haiba kaongeya.*

Ubeti huu unatubainishia kuwa Liyongo alikuwa mwanamume aliyependa ukweli. Alikuwa mtu mwenye tabia njema.

Katika *Kifo Kisimani*, Mwelusi pia anasawiriwa kama kijana mwadilifu. Uadilifu huu unajitokeza katika mzungumzo haya:

*Mwelusi: .... La! Siwezi kuwaambia watu kwamba nimeacha uchochezi. Mtu hawezi kuacha jambo ambalo hajaanza bado. Siwezi kusema kwamba majirani wana mipango ya kuvuruga amani na maendeleo katika Butangi. Ikiwa majirani wana mipango hiyo, sina habari.*

*Batu: Ulimaanisha nini uliposema kwamba unaipenda Butangi kwa dhati? Huwezi kuipenda Butangi huku ukijihusisha na mambo ya kutatiza maendeleo.*

*Mwelusi: Sijihusishi na mambo ya kutatiza maendeleo*

*Batu: Pale mwanzo, nilisema sitakuuliza kama wewe nimiongoni mwa kundi la waharibifu la Kabakaba. Kuna ushahidi wa kutosha wa kudhibitisha jambo hilo.*

*Mwelusi: Mimi si mharibifu. Simo katika kundi lolote la waharibifu.*

(uk 31)

Kutokana na mazungumzo haya, inabainika kuwa Mwelusi alikuwa kijana mwadilifu aliyeipenda nchi yake kwa dhati. Aidha, mifano tuliyotoa hapo juu inaonyesha matendo ya wahusika hawa yalikuwa yenye maadili mema.

Wahusika hawa pia wamependwa na wengi. Katika beti za 225 - 227, tunaona kuwa Liyongo alipofariki, watu walisikitika na kuhuzunika sana. Walikuwa wamemchukua kama ngao dhidi ya maadui wao. Waliweka matanga kwa maombolezi na masikitiko mengi. Mwelusi alipotiwa gerezani, watu wengi walikuja wakiimba. Askari walipowaona, walitoroka na watu wale wakaja na kumchukua Mwelusi kutoka gerezani. Vilevile, alipofariki, watu aliokuwa amewazindua walikuja kulipiza kisasi kwa Bokono na wafuasi wake. Waliwashika na kuwapeleka gerezani na hivyo, kuuporomosha uongozi dhalimu wa Bokono. Hii ni ishara ya jinsi wahusika hawa walivyopendwa na watu wa jamii zao.

Aidha, familia za Liyongo na Mwelusi zilikuwa chini ya uongozi wa mama pekee. Habari za babake Liyongo hazijatolewa katika utenzi. Katika tamthilia, tunaarifiwa kuwa babake Mwelusi alikuwa ameaga dunia hapo mbeleni. Hivyo, mashujaa hawa wawili, wamekua chini ya malezi ya mama zao tu.

Mhusika Mwelusi amesawiriwa kama mhusika Liyongo wa *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Mengi ya yale yaliyompata ni kama yale yaliyompata mhusika Liyongo. Kwa mfano, alichukiwa na Bokono, akatiwa gerezani, akafungwa kwa minyororo ndani ya gereza, akiletewa chakula kilikuwa kikiliwa na askari walinda mlango wa gereza. Hatimaye, alipofaulu kutoroka gerezani baada ya kuletewa tupa ikiwa ndani ya mkate wa wishwa, aliitumia kuikata minyororo yake akawa huru. Hata hivyo, mtego uliwekwa upya na wakati huu, akaishia kuuawa na kakake. Tunaposoma matukio haya, yanatukumbusha mhusika Liyongo kwani hata naye aliyapitia yayahaya na mwishowe akauawa na mwanawe wa kiume. Hivyo, ni bayana kuwa Wa Mberia alimsawiri mhusika Mwelusi kama mhusika wa kitendi na hasa, mhusika Liyongo.

**Mfalme na Bokono**

Mfalme alikuwa kiongozi wa Pate naye Bokono alikuwa kiongozi wa Butangi. Kulingana na matendo na maneno yao, tunabaini kuwa, wahusika hawa wanaingiliana kisifa. Bokono na Mfalme ni viongozi wenye tamaa ya uongozi. Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* (ubeti wa 51), inadhihirika kuwa, Mfalme aliogopa Liyongo angemnyang'anya ufalme na hivyo, akapanga kumwondoa duniani. Katika *Kifo Kisimani* (uk 10), Bokono anasema kuwa ni Mungu aliyemfanya kiongozi wa Butangi. Naye Zigu anamwambia kuwa yeye, Bokono, angeongoza

Butangi kwa miaka mia moja. Tamaa hii ya uongozi ndiyo inayomfanya Bokono kutokuwa na amani hasa anaposikia kuwa kulikuwa na watu waliokuwa wakipinga uongozi wake. Aidha, kiongozi huyu anasema kuwa hangewaruhusu watu wachache kuutia nyufa uongozi wake. Watu hawa, wanadhaniwa kutia nyufa kwenye uongozi, wangekomeshwa kabisa. Tamaa hii ndiyo iliyowafanya wahusika waliodaiwa kuwa wapinzani kuuawa na tawala husika.

Aidha, viongozi hawa ni dhalimu. Mfalme alikuwa mtu dhalimu. Kule kumwonea Liyongo wivu na kuogopa kwamba angempokonya ufalme pia ni udhalimu. Hataki kuona mwingine na mazuri. Yeyote aliyeonyesha ushindani wa kisiasa kwa nama yoyote ile aliuawa. Alimuua Liyongo kwa kuogopa kuwa angempokonya ufalme siku moja. Hakutaka upinzani, alitaka kuwatawala watu atakavyo daima. Bokono pia alikuwa dhalimu. Aliwatesa na kuwaua wale waliopinga uongozi wake. Mwelusi aliuawa kwa kuwa alionekana kama tisho katika utawala wa kiongozi huyu. Mtemi Bokono hakuwa tayari kuuachilia uongozi, hivyo, aliyeonekana kulizima azimio hili, kama vile Mwelusi, aliishia kuangamizwa ili kukomesha upinzani milele.

Bokono na Mfalme vilevile ni wauaji. Wote waliamini kuwa walipaswa kuongoza daima na hakuna mwingine angeweza kuchukua nafasi zao. Kwa sababu hii, yeyote aliyeonyesha dalili ya kuwashinda viongozi hawa hasa kiumaarufu, aliweza kukomeshwa na kuzimwa kwa kutolewa uhai. Viongozi hawa walihusika moja kwa moja kwa mipango ya mauaji ya wapinzani wao.

**Mwana wa Liyongo na Gege**

Wahusika hawa wamesawiriwa kama wasaliti. Mwana wa Liyongo alijifanya mzuri kwa babake ili ampe siri ya kile kingeweza kumuua. Babamtu alimwamini ila hakujua mwana huyu ndiye angekuja kumwondoa duniani. Pia, Gege alijifanya kubadili msimamo wake kuhusu kakake. Nduguye akamwamini bila kujua kuwa yeye ndiye angemuua baadaye. Wahusika hawa walipaswa kuwalinda wendani wao lakini walibadilika na kuwa wasaliti na kuwaua watu waliopaswa kuwalinda.

Vilevile, wahusika hawa ni wenye tamaa ya mali. Walishawishika kwa urahisi na ahadi za kuozwa mabinti wa viongozi wao. Waliona kuwa ndoa ya aina hiyo ingeleta mambo mengi mazuri na utajiri wa haraka. Kwa sababu ya tamaa hii, wahusika hawa walitekeleza mauaji lakini baadaye wakaambulia patupu kwani ahadi zenyewe, zote zilikuwa za uongo.

Vijana hawa pia ni wauaji. Mwana wa Liyongo alimuua babake ili kutimiza amri ya Mfalme naye Gege alimuua kakake ili atimize amri ya kiongozi Bokono. Vijana wote hawa, waliongozwa na tamaa ya mali na umaarufu ndipo waliweza kutimiza maovu haya. Usawiri wa wahusika hawa umefanyika kimwingilianomtini. Wahusika hawa wanajitokeza takriban kama mhusika mmoja mwenye jina tofauti katika tamthilia. Hii ni kwa sababu wahusika hawa walipewa nafasi inayoshahiana kwa karibu sana katika kazi zote mbili. Mfano, vijana hawa walikuwa bado hawajaoa, wote waliahidiwa ndoa za mabinti wa viongozi miongoni mwa mambo kadha mazuri waliyoahidiwa. Walishawishika kwa urahisi pasi na kujua kuwa ulikuwa uongo mtupu. Waliwaua wapendwa wao kwa kuwadunga kwa vifaa kali tumboni na kuwaua. Baadaye wote waliambulia patupu kwani ahadi walizokuwa wamepewa hazikuwa za kweli. Hivyo, ni bayana kuwa, kuna mwingilianomatini katika usawiri wa wahusika Gege na Mwana wa Liyongo.

**Askari**

Askari wametumika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani*. Walijitokeza kama watu walafi. Walikataa kuwapelekea wafungwa vyakula walivyoletewa na wapendwa wao na badala yake, walikuwa wakila chakula hicho. Aidha, ni watu wasiokuwa na utu. Waliwafunga wafungwa kwa minyororo na kuwafungia gerezani na zaidi ya hayo, waliwachunga mlangoni wasije wakatoroka. Huu ni unyama waliotendewa watu hawa hasa ikizingatiwa kuwa, haya yote yalitendeka kwa watu ambao hawakuwa wamethibitishwa kuwa na hatia yoyote. Hata kule kuwanyima wafungwa chakula na kitendo cha ukosefu wa utu. Waliwatesa kwa njaa ilhali chakula chao kilikuwa kimeletwa na wapendwa wao.

**Tanya, Atega na Mamake Liyongo.**

Tanya alikuwa mamake Mwelusi naye Atega alikuwa rafikiye Mwelusi waliyeshirikiana naye katika harakati za ukombozi. Watatu hawa ni wanawake waliosawiriwa kwa namna inayolandana.Tanya na Mamake Liyongo ni walezi wema. Wanawalea mashujaa hawa, Mwelusi na Liyongo, vyema. Malezi waliyowapa yaliwafanya kuwa na tabia njema na kwa hivyo, kuwa vipenzi vya wengi katika jamii zao. Hawa wahusika walitia bidii katika ulezi wa wanao. Vilevile, wanawapenda wanao kwa dhati. Liyongo na Mwelusi wanapotiwa gerezani, mama zao

wanafanya juhudi kuwapikia chakula kizuri. Hata kinapokosa kuwafikia kwa sababu ya kuliwa na askari, hawakati tamaa, wanapika tena na tena. Haya ni mapenzi makuu kwa wanao.

Wahusika hawa walikuwa werevu. Mamake Liyongo na Atega walitengeneza mkate wa wishwa na kutia tupa ndani yake. Huu ni ujuzi wa juu kwani hata askari hawakuweza kuona hiyo tupa. Tupa hii ndiyo Liyongo na Mwelusi waliyoitumia kuikereza minyororo waliyokuwa wamefungwa kwayo na hivyo, wakawa huru. Wanawake hawa pia ni wakakamavu. Mamake Liyongo alionyesha ukakamavu alipotumana na mkate uliotiwa tupa upelekewe Liyongo gerezani. Atega ndiye aliyeutengeneza mkate uliomsaidia Mwelusi kutoroka gerezani. Alipeleka mkate huu kwa ukakamavu, hakuogopa kuwa askari wangegundua ujanja ule. Uerevu huu ulimfaa sana Mwelusi.

**Alida na Bintiye Mfalme**

Wahusika hawa wametumika kimwingilianomatini kama kishawishi cha kufanya vijana wa kiume, Gege na Mwana wa Liyongo, kutekeleza mauaji. Gege aliahidiwa kuozwa Alida ambaye alikuwa bintiye Bokono, pindi tu anapofanikiwa kumuua Mwelusi. Naye Mwana wa Liyongo akaahidiwa kuozwa bintiye Mfalme iwapo angefanikiwa kumuua Liyongo. Mabinti hawa, wametumika kusawiri maudhui ya nafasi ya mwanamke katika jamii kwani wanatudhihirishia kuwa, wazazi wa kiume ndio tu walikuwa na uwezo wa kuamua yule angeoa binti yake na binti huyu kamwe hangepinga uamuzi huu.

Matendo ya wahusika tuliowajadili hapo juu yamedhihirisha wazi sifa zao. Matendo ya wahusika wa *Kifo kisimani*, yalishabihiana na yale ya wahusika wa *Utenzi wa Fumo Liyongo* na hivyo, wahusika hawa, kwa pamoja, wakawa na sifa sawa. Usawiri huu hivyo basi, umefanyika kimwingilianomatini. Mifano tuliyojadili hapo juu inaonyesha bayana kuwa, Kijumwa na Wa Mberia waliwasawiri wahusika wao kwa njia zinazolandana. Wahusika wa *Kifo Kisimani* (tuliowaangazia hapo juu) walisawiriwa kimwingilianomatini kwani tunaweza kulinganisha sifa zao na zile za wahusika wa *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Kwa vile utenzi teule ndio kazi ya awali, basi tunaposoma tamthilia teule na kukumbana na wahusika tuliowajadili hapo juu, tunakumbuka wahusika teule katika kazi hii ya awali ambayo ni *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Bila shaka,

mwingilianomatini katika usawiri wa wahusika umejidhihirisha wazi katika kazi zote mbili tulizozitafiti.

### 3.4 Mwingiliano katika Usawiri wa Mandhari

Allen (200:23) akimnukuu Bakhtin anasema kuwa, usemezano sio mazungumzo baina ya wahusika katika kazi ya fasihi. Usemezano ni ile hali ambapo matini 'huzungumza' kwa kuonyesha kuwepo kwa matini za awali zilizoko ndani yake. Hivyo, tunaposoma kuhusu mandhari fulani katika matini fulani ya kifasihi na kuweza kuyahusisha na mandhari ya aina hiyo katika kazi nyingine ya awali, basi hali hii inaweza kudhihirisha sifa ya mwingilianomatini katika kazi husika. Kijumwa na Wa Mberia wametusawiria mandhari inayolandana. Wamesawiri mandhari ya kijiografia na vilevile, mandhari ya kiwakati.

#### 3.4.1 Mandhari ya Kijiografia

Kisimani ni mandhari inayoonekana kujitokeza katika katika kazi zote mbili. Mandhari hii imeonekana kuhusishwa sana sana  na sehemu za vijijini. Watu wengi katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* walitegemea maji ya kisima. Hata Liyongo alipokwamia kisimani, akionekana kama alikuwa tayari kwa mashambulizi, watu walikaa siku tatu bila maji na wakateseka sana. Mamake alienda kisimani mara kadha kumshawishi aondoke kisimani, ila hakuonyesha kumsikia mamake kwa vile hakuondoka hapo. Baadaye, alipoanguka pale, ndipo walibaini kuwa alikuwa amefariki. Kwa upande mwingine, watu wengi katika *Kifo Kisimani* walitegemea maji ya Kisima cha Mkomani. Hata utawala wa Bokono ulipopiga kisima hiki marufuku kwa matumizi ya umma, watu waliteseka. Hii ndiyo ilikuwa mojawapo ya sababu ya Mwelusi kuanzisha mapambano ya ukombozi. Matukio ya onyesho la tisa, yanafanyika kisimani. Mwelusi anapofika nyumbani kutoka gerezani, anaambiwa kuwa dadake, Andua, alikuwa ameenda kuteka maji kisimani. Kwa sababu ya hatari iliyotokana na kuvunja sheria ya kutoteka maji kwenye kisima hiki, Mwelusi aliamua kumfuata dadake ili ahakikishe kuwa alikuwa salama. Gege alimfuata na baada ya kumshawishi waende chemba, alimdunga Mwelusi tumboni kwa kisu, akaanguka na kufia kisimani. Mandhari hii imetumika kuonyesha athari za uongozi mbaya katika jamii zote mbili zilizolengwa na Kijumwa na Wa Mberia. Aidha mandhari hii imesawiriwa kimwingilianomatini kwani imejitokeza kuwa na umuhimu mkubwa sana katika pande zote mbili.

Kuna pia mandhari ya ikuluni. Tumetumia neno hili kurejelea makao rasmi ya viongozi katika kazi tulizozitafiti. Viongozi katika kazi teule, walikuwa na makao yao rasmi ambapo waliendeleza shughuli za nchi zao husika. Wagala waliposema walitaka kumwona Liyongo, Mfalme alitumana ili aitwe. Liyongo alifurahi na akasafiri hadi mjini, akakaribishwa ikuluni. Wagala walipomwona, walitamani awe wao na hivyo, wazo la kumwoza binti yao ili azae mwana kama yeye (Liyongo), likazuka. Wazo hili lilijadiliwa kwenye makao rasmi ya Mfalme na liliweza kutekelezwa. Vilevile, Mfalme alipomwita mwana wa Liyongo ili amshawishi kumuua babake, matukio haya yalifanyika kwenye makao haya ya uongozi. Hata anapomfukuza kijana huyu baada ya kumuua babake, walikuwa ikuluni.

Kwa upande mwingine, Bokono alikuwa na ikulu pia. Matukio ya onyesho la saba na la kumi yanafanyika katika Ukumbi wa Utawala wa Butangi. Mambo muhimu yalipangiwa hapa. Katika onyesho la saba, Batu na wenzake wanapanga jinsi watakavyomuua Mwelusi alipokuwa gerezani. Wanajadili mbinu tofauti ambazo wangetumia kumuua. Kwa bahati mbaya, wanaarifiwa kuwa mfungwa alikuwa ametoroka gerezani. Mweke na Talui wanapewa jukumu la kumtafuta na kummaliza. Hapa ndipo wazo la kumtumia Gege, kumuua kakake, linatokea. Katika onyesho la kumi, Gege anakuja na ujumbe kuwa alikuwa amemuua Mwelusi na hivyo, mwiba ulikwa ushaondoka kwenye mguu wa Butangi. Hata hivyo, hakuzawadiwa kama alivyotarajia na alipoonyesha kutoridhika, alitolewa nje ya ukumbi kwa nguvu. Tamthilia inaisha pale wananchi waliozinduka wanawavamia Bokono na wafuasi wake ikuluni, wakawafunga na kuwapeleka gerezani. Mwingilianomatini unajitokeza katika usawiri wa mandhari hii kwa vile jamii zote mbili zina viongozi waliokuwa na makao rasmi. Maamuzi muhimu yameonyesha kufanyiwa ikuluni na kutekelezwa kwa kufuata amri za kiongozi.

Gereza pia imejitokeza kama mandhari muhimu katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani*. Mandhari hii ilitumika na viongozi wa pande zote mbili kuwaadhibu watuhumiwa wa upinzani. Liyongo na Mwelusi walitiwa gerezani, wakafungwa kwa pingu na minyororo na askari wakawekwa kulinda mlango wa gereza ili wafungwa wasitoroke. Imejitokeza pia kuwa, wafungwa wakati mwingine, waliuawa wakiwa gerezani kwani katika kazi zote mbili, tunaona mijadala kuhusu jinsi ya kukabiliana na waharibifu hawa. Kwa mfano, Mfalme na washauri wake walijadili vile wangemfanya Liyongo alipokuwa gerezani, mwishowe, Mfalme akaamua

amuue kwani hakutaka kumwachilia kisha ajute baadaye. Kwa upande mwingine, Batu ambaye alikuwa mshauri mkuu wa Bokono, na wenzake walijadili njia mbalimbali ya kumtuliza Mwelusi alipokuwa gerezani. Mwishowe, walikubaliana auawe ili shida hii iwaondokee kabisa. Hata hivyo, wafungwa hawa, wanafaulu kutoroka gerezani kwa kutumia mbinu sawa kwani walitumia tupa, iliyoletwa ikiwa ndani ya mkate wa wishwa, kuikereza minyororo yao na hivyo, wakawa huru. Mandhari hii pia inadhihirisha mwingilianomatini kwani matukio yaliyotokea gerezani yanafanana sana ingawa kazi hizi zimeandikwa na waandishi tofauti na kipindi tofauti cha wakati.

Mandhari za kijiografia zilizoswawiriwa na Kijumwa na Wa Mberia zimeonyesha mshabaha mkubwa. Mshabaha huu ni kuwa, wahusika hawa walifungwa gerezani ingawa walifaulu kutoroka wakitumia mbinu sawa. Hata hivyo, waliuawa na wapendwa wao na wote walifia kisimani. Maamuzi haya yote yameonekana kufanyika ikuluni kwani viongozi walikuwa na nafasi muhimu katika mipango ya maendeleo ya jamii husika. Hivyo, mwingilianomatini umejitokeza wazi katika aina hii ya mandhari.

### 3.4.2 Mandhari ya Kihistoria

Mandhari hii imejitokeza katika kazi hizi mbili tulizozitafiti. Ikizingatiwa kuwa *Utenzi wa Fumo Liyongo* uliandikwa mwanzo wa karne ya ishirini, ambapo miundo msingi haikuwa imeimarika na pia matumizi ya teknolojia hayakuwa maarufu miongoni mwa Waafrika, tunaweza kusema kuwa, mambo yaliyotendeka wakati huo yalikuwa ya wakati wa zamani. Kwa mfano; hakukuwa na matumizi ya simu. Wajumbe walitumwa mahali mbalimbali kupeleka jumbe. Kuna mjumbe aliyetumwa na Mfalme kwa Liyongo na mtu huyu alisafiri hadi alikokuwa ametumwa kupeleka ujumbe huu. Vilevile, hakukuwa na magari ya usafiri. Watu walisafiri mwendo mrefu kwa miguu. Liyongo alipokuwa akielekea Pate kuitika ujumbe wa Mfalme, alienda kwa siku mbili ingawa tunaambiwa kuwa hiyo ilikuwa safari ya siku nne. Watu pia hawakuwa na maji ya mabomba, walitumia maji ya kisima, kilichokuwa kimoja tu, kukata kiu chao. Aidha, watu walijiburudisha kwa kutumia michezo ya ngoma. Tunaambiwa kuwa Liyongo aliipenda ngoma sana na alikuwa hodari kwa gungu. Vilevile, askari walipomkamata Liyongo walitumia ala za zamani za kulinda usalama kama vile; mishale, mikuki na magongo. Pia, kule kumfunga Liyongo kwa minyororo gerezani ni ishara ya mambo ya kihistoria. Zaidi ya hayo, wanawake

hawakupewa nafasi ya uongozi na hawakuwa na usemi wowote mbele ya wanaume. Hii ndio sababu, Mfalme anaamua ni nani angemwoa bintiye na binti huyu hangekataa kamwe amri ya babake. Desturi hii pia ilijulikana na wanajamii na ndiposa mwana wa Liyongo aliamini maneno haya upesi.

Katika karne hii ya ishirini na moja, takribani karne moja tangu *Utenzi wa Fumo Liyongo* ulipoandikwa, mambo yamebadilika sana. Kuna miundo msingi iliyoimarika na pia teknolojia imepevuka. Siku hizi kuna matumizi ya simu. Kwa sababu hii, watu hawaendi mwendo mrefu kupeleka ujumbe. Wao hupitisha jumbe zao kupitia simu. Vilevile, kuna magari ya usafiri na hivyo, mwendo uliokuwa wa siku kadha, watu wanatumia saa chache wanafika walikokuwa wakienda. Askari siku hizi wanatumia silaha zilizopevuka. Kuna matumizi ya bunduki kulinda usalama. Hakuna tena matumizi ya minyororo kuwafungia wahalifu. Hata wanapofungwa kwa pingu, sio wakiwa ndani ya gereza bali wakiwa nje. Hali kadhalika, kuna maji ya mabomba na ingawa kuna wale wanaotumia maji ya visima, sio kuwa ni nchi nzima. Uchezaji wa ngoma za kienyeji pia unafifia sana. Hii ni kwa sababu watu huenda kwenye disko wanapohitaji kujiburudisha kwa mziki na ngoma.

Licha ya kuwa mambo yamebadilika sana kama tulivyojadili hapo juu, Wa Mberia amesawiri mandhari ya kiwakati yanayoshabihiana na yale yaliyosawiriwa na Kijumwa. Kwa mfano; Matumizi ya dhana ya "Mtemi" ikirejelea kiongozi wa nchi mwenye hadhi sawa na mfalme. Dhana hii haitumiki katika jamii ya sasa, hasa katika jamii ya Afrika Mashariki ambapo *Kifo Kisimani* inaaminika kuwa zao la mfumo wa tamaduni za jamii hii. Dhana hii, ilitumika kimwingilianomatini. Aidha, Kaloo anatumwa kuwaita watu waliokuwa wameambiwa wangoje Mingamiwili hadi uwanja wa mkutano utakapomalizia kutayarishwa. Kaloo alipoenda, hakuwapata kama alivyotarajia. Alirudi kumwambia Batu habari hiyo. Haya ni matumizi ya wajumbe kama waliotumika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Vilevile, watu wanasafiri kwa miguu kwa shughuli zao za kila siku. Hatukuona matumizi ya magari licha ya kuwa magari yanatumika katika karne hii ya ishirini na moja.

Mwelusi alipokamatwa, alifungwa kwa minyororo kama vile Liyongo alivyofungwa. Askari walitumia silaha za zamani kama vile mikuki katika ulinzi wao. Katika ukurasa wa 59, Askari II anatuambia kuwa mikuki ilikuwa imechukuliwa na mnoaji na hakuwa ameirudisha. Hii ni baada

ya kuona watu waliokuwa wanaelekea walikokuwa askari hawa huku wakiimba. Walibaini kuwa, walikuwa wanakuja kumwokoa Mwelusi ambaye tayari alikuwa ashakata minyororo yake na hivyo, wakaona kuwa walikuwa hatarini. Hivyo, Askari III anamwambia Askari II aendee mikuki ili wajilinde nayo dhidi ya umati, na ndipo mwenzake anampa jibu hili. Wanabutangi pia walitumia maji ya kisima. Hakuna mahali maji ya mfereji yalionekana kutumika na jamii hii. Ngoma pia ilitumika katika tamthilia teule kwa burudani. Kaloo anasema kuwa wangecheza Chakacha kumburudisha Mtemi wakati wa mkutano. Aidha, Tanya anasemekana kuwa hodari kwa uchezaji wa ngoma na mwanawe, Gege, pia ana talanta hii ya kutengeneza ala za muziki na kucheza ngoma. Pia, Gege anaambiwa kuwa Mtemi alikuwa amesema kuwa angemwoza bintiye iwapo angemuua kakake. Hili linamaanisha kuwa wazazi, na hasa kina baba, ndio walioamua nani angeoa mabinti zao na wasichana hawa hawangekataa agizo la baba zao.

Huu ni mshabaha mkubwa wa mandhari hii ya kihistoria. Kazi zote zimesawiri mambo yaliyofanyika enzi za zamani ambapo hakukuwa na matumizi ya teknolojia mpya miongoni mwa wanajamii. Kwa vile *Kifo Kisimani* iliandikwa karne ya ishirini na moja, tungetarajia kuona mambo yanayohusishwa na usasa. Mambo haya ni kama vile, matumizi ya magari ya usafiri, matumizi ya simu, elimu kwa vijana kama chombo cha uzindushi, mwanamke aliyeelimika na kupewa nafasi mbalimbali za uongozi, matumizi ya silaha pevu za ulinzi na vilevile, matumizi ya maji ya mabomba. Kwa vile mambo yanayojitokeza katika tamthilia hii ni kama tu yale yanayotokea katika utenzi teule, basi ni bayana kuwa imesawiri mandhari ya kihistoria inayoshabihiana na ile ya *Utenzi wa Fumo Liyongo* na hivyo, ni wazi kuwa, mwingilianomatini unajidhihirisha katika kiwango hiki cha mandhari. Kwa jumla, kama tulivyofafanua katika sehemu hii ya mandhari, ni wazi kuwa Kijumwa na Wa Mberia, wamesawiri mandhari inayoshabihiana kwa kiasi kikubwa. Hivyo basi tunaweza kusema kuwa, kuna mwingilianomatini katika kiwango hiki cha mandhari.

### 3.5 Mwingiliano wa Kiusimulizi

Miongoni mwa mambo ambayo mwandishi anaweza kuiga kutoka kwa kazi za awali ni ploti na mbinu za usimulizi Allen (2000:11). Hili lina maana kuwa, tunaweza kupata matini zinazoakisiana katika vitushi na jinsi matukio hayo yanayosababishana ili kukuza maudhui na dhamira ya mwandishi. Aidha, matukio hayo pia yanaweza kutokea katika mazingira sawa. Hali

kama hii inapotokea, basi kazi hizi zitakuwa na mwingilianomatini katika kiwango cha usimulizi. Katika sehemu hii tutajadili vipengele vya ploti na matumizi ya nyimbo na ngoma na jinsi vilivyotumika kimwingilianomatini kukuza maudhui na dhamira katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani*.

### 3.5.1 Mwingiliano wa Ploti katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani*

*Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* zinashabihiana kimsuko. Wahusika wakuu wote wawili ni vijana wa kiume. Wote wamelelewa katika familia zilizokuwa na mama pekee. Baba wa Liyongo hakuelezwa alikokuwa naye babake Mwelusi alisemekana kuwa alikuwa amefariki. Mama za mashujaa hawa wamepewa jukumu la kuwalea na kuwatunza. Mwelusi na Liyongo wamesawiriwa kama watu wenye adabu njema na waliowaheshimu na kuwasikiliza mama zao sana. Vilevile, wahusika hawa walikuwa na umaarufu na walipendwa na wengi. Hali hii ndiyo iliyowafanya viongozi wao kuwaogopa kuwa wangewanyang'anya uongozi siku moja na hivyo, wakapanga kuwaangamiza. Wote wanashikwa, wanafungwa kwa pingu na minyororo na kutiwa gerezani. Walipopelekewa chakula, askari walikuwa wakila kisiwafikie chakula chochote. Walipokuwa gerezani, mijadala ya jinsi ya kukabiliana na wafungwa hawa ilikuwa ikiendelea ikuluni. Uamuzi uliafikiwa kwamba wafungwa hawa wauawe ili kuzima upinzani wao wa kisiasa.

Askari katika kazi hizi mbili walitumia ala za kulinda usalama zinazofanana. Baadhi ya silaha ambazo askari, wanaorejelewa katika utenzi kama "majuma", walikuwa nazo wakati wa kumkamata Liyongo ni mikuki, inayorejelewa katika utenzi kama "mafumo". Aidha, walimfunga Liyongo kwa pingu na minyororo ili asiweze kutoroka. Vilevile, askari wa *Kifo Kisimani* walitumia mikuki kulinda usalama na pia walimfunga Mwelusi kwa pingu na minyororo ili asitoroke gerezani. Hata hivyo, wote walifaulu kutoroka gerezani kupitia kukata minyororo, waliyokuwa wamefungwa kwayo, kwa tupa walizokuwa wameletewa zikiwa ndani ya mikate ya wishwa iliyoletwa na wapendwa wao. Mkate huu ulidharauliwa na askari wa pande zote mbili kuwa ni wa watu wa hadhi ya chini kama wahusika waliokuwa gerezani. Hivyo, waliwapelekea na hivyo ndivyo wafungwa hawa walijipatia uhuru wao.

Wanapofaulu kutoroka, viongozi katika kazi zote mbili, hawakuonyesha kukata tamaa. Wanawatumia jamaa za washukiwa kutekeleza maovu. Jamaa hawa wawili walikuwa vijana wa

kiume. Waliahidiwa kuozwa mabinti wa viongozi ili washawishike kwa urahisi. Walishawishika na wakawaua wapendwa wao. Mwelusi aliuawa na Gege ambaye alikuwa kakake, naye Liyongo aliuawa na mwanawe. Wahusika hawa walifariki kwa njia inayolandana. Wote walidungwa tumboni, Liyongo alidungwa sindano ya shaba kitovuni naye Mwelusi akadungwa kisu tumboni, na walifia kisimani.

Vijana wauaji wote waliambulia patupu licha ya kuwaua wapendwa wao. Gege alipodai ahadi ya kuozwa bintiye Mtemi Bokono, alichukuliwa kuwa mlevi au aliyekuwa katika ndoto, mbele ya mtemi na watu wake. Hatimaye anaishia kutolewa mbele ya Mtemi kwa nguvu. Mwana wa Liyongo vilevile hakupata kitu. Kijana huyu alipofika mbele ya mfalme akitaraji kupokea zawadi yake, baada ya kumuua babake, mfalme alimgeuka. Alimfukuza kwake bila chochote. Ahadi walizoahidiwa vijana hawa ziliishia kuwa za uongo.

Vifo vya Liyongo na Mwelusi viliwahuzunisha wengi kwa mapenzi waliyokuwa nayo kwao. Mwana wa Liyongo aliporudi nyumbani alitengwa na jamaa zake. Aliishi kwa upweke mwishowe akafariki. Gege naye alipomuua Mwelusi, alikamatwa na watu waliokuwa na ghadhabu na kutiwa gerezani. Hapa pia naye alitengwa na jamaa zake na kuishi maisha ya upweke humo gerezani. Jambo lililowazi ni kuwa, vijana hawa hawakukubalika katika jamii zao tena kutokana na vitendo walivyovitenda.

Matukio katika kazi hizi yameelezwa kwa mtindo sahili. Matukio mengi yamefuatana moja kwa moja yakisababishana. Hivyo, tunaweza kusema kuwa zote zina ploti sahili. Kuna pia matumizi ya usimulizi wa mwandishi na ule wa wahusika. Usimulizi wa wahusika umetumika kwa kina kwenye tamthilia lakini pia kuna maelekezo tunayopewa na mwandishi na hayo yanaingia katika kitengo cha usimulizi wa mwandishi. Mwandishi wa utenzi pia ametumia mbinu hii. Kuna sehemu ambazo sauti yake inasikika; mfano, ubeti wa 1-9 na sauti ya mhusika inasikika kutoka ubeti wa 12-15. Hivyo, kuna mwingilianomatini katika mitindo hii ya usimulizi.

### 3.5.2 Mwingiliano katika matumizi ya nyimbo na ngoma

Jamii zilizosawiriwa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* zinapenda nyimbo na ngoma sana. Mara nyingi, ngoma huandamana na nyimbo. Katika ubeti wa 77, tunaambiwa kuwa Liyongo alikuwa shaha wa gungu na mwao na aliwashinda wote kwa mambo haya;

mambo ya ngoma, uimbaji na utungaji. Gungu na mwao ni ngoma za zamani zilizochezwa na watu wa mwambao wa Afrika ya Mashariki. Liyongo alikuwa hodari na mkubwa wa ma-shaha wengine. Usiku ule akiikereza minyororo, watu walikuwa wakicheza ngoma na kujisahau, wakagutuka kumwona katikati yao. Katika *Kifo Kisimani*, Kaloo anaeleza jinsi wangemkatikia Mtemi na kutingisha viuno. Mojawapo ya ngoma ambayo wangeicheza ilikuwa ni Chakacha. (UK 3-4). Vilevile, Tanya anasemekana kuwa mchezaji ngoma hodari na mwanawe, Gege, alikuwa karithi talanta hii. Gege alitengeneza ala za mziki, aliimba na kucheza ngoma. Hata anaringa vile wasichana katika uwanja wa ngoma wangemtambua pindi tu anapoingia uwanjani na kwamba wangejua kuwa yeye alikuwa mtoto wa Tanya (uk 44). Pia, umati uliokuwa unakuja kumwokoa Mwelusi ulikuja ukiimba. Wimbo huu ndio uliowatia moyo wa kipigania haki yao, na hili liliwatia askari hofu na kutoroka ili kuokoa maisha yao. Hali iliwafanya waweze kumfungulia Mwelusi kutoka gerezani.

Nyimbo na ngoma ni vipera vya fasihi simulizi vinavyotumika kuburudisha watu na vilevile kuwatia moyo wanapofanya jambo fulani ili kuondoa uchovu. Mbinu hizi zimetumika kimwingilianomatini na mwandishi wa *Kifo Kisimani* ikizingatiwa kuwa, ngoma ni kipera kinachoonyesha kupitwa na wakati katika kipindi cha sasa kwa sababu ya upevu wa teknolojia. Hivyo, kuna mwingilianomatini katika matumizi ya kipengele hiki cha usimulizi.

**Mahitimisho**

Katika sura hii tumejadili mwingilianomatini katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* katika viwango vya kimaudhui, uhusika mandhari na pia usimulizi. Tumebaini kuwa, Kijumwa na Wa Mberia wamesawiri maudhui yanayolandana katika kazi zao tulizozitafiti. Hii ni ishara kuwa, jamii zilizolengwa na waandishi hawa ziliathiriwa na masuala takriban yaliyo sawa na hivyo, kazi hizi zao zikalenga kuyashughulikia.

Aidha, tumetambua kuwa wahusika wamesawiriwa kwa mbinu zinazoshabihiana. Wahusika wengi wamelandana kisifa na bila shaka ndio sababu wanakuza maudhui yanayoshabihiana pia. Hivyo, waandishi hawa walifanikiwa kusawiri wahusika wao kimwingilianomatini na hivyo, kudhihirisha sifa ya mwingilianomatini katika kazi hizi tulizozitafiti.

Vilevile, tumeona kuwa mandhari yamesawiriwa kwa njia inayoshabihiana. Katika kazi zote mbili, kuna mandhari ya kijiografia na vilevile mandhari ya kihistoria. Mandhari haya yaliwakuza wahusika wa kazi hizi kisifa. Mfanano huu unasaidia kukuza maudhui ya kazi husika ambayo pia yanalandana. Kwa sababu hii, tunaweza kusema kuwa, kuna mwingilianomatini katika kiwango hiki cha mandhari.

Hali kadhalika, usimulizi unajitokeza kwa njia ya mwingilianomatini. Ploti za kazi hizi ni sahili na matukio yanafanana kwa kiwango kikubwa. Tumeona pia kuna matumizi ya nyimbo na ngoma katika kazi zote mbili. Vipera hivi vya fasihi simulizi vimetumika kutekeleza kazi sawa; ile ya kuburudisha na kutia moyo au kuliwaza.

Matokeo haya yametuelekeza kuafikia lengo letu la pili ambalo lilikuwa, kuchunguza jinsi *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* zinavyoingiliana katika viwango vya maudhui, uhusika, mandhari na usimulizi. Maelezo haya yanajibu swali letu la pili kuwa, kuna mwingilianomatini katika kazi teule na mwingiliano huu unadhihirika katika viwango vilivyotajwa hapo juu.

# SURA YA NNE

# ATHARI ZA MWINGILIANOMATINI KATIKA UDHAMIRISHAJI NA MTINDO WA TAMTHILIA YA *KIFO KISIMANI*

## 4.1 Utangulizi

Nadharia ya mwingilianomatini husisitiza kuwa, matini haiwezi kujitosheleza kimaana bila kuhusishwa na matini nyingine ya awali inayohusiana nayo. Hii ina maana kuwa, mwandishi wa matini fulani haandiki kazi yake kutoka kwa ombwe tupu. Yeye huchota mambo fulani kutoka kwa matini nyingine za awali. Mambo haya yanaweza kuwa uhusika, mbinu za usimulizi, ploti, masuala ya kushughulikia pamoja na lugha ya kutumia miongoni mwa mengine (Allen 2000:1, 12). Hivyo, ni bayana kuwa, kazi ya awali huiwekea kazi ya baadaye misingi ya mifumo ya kanuni na tamaduni mbalimbali.

Tamthilia ya *Kifo Kisimani* imefaidi kwa namna moja au nyingine kutokana na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Hali hii imewezeshwa na ukweli kwamba, kuna mwingilianomatini baina ya kazi hizi mbili. *Kifo Kisimani* imeakisi utenzi teule kwa kiwango fulani kama tulivyoonyesha katika sura ya tatu. Kwa vile utenzi huu ndio kazi ya awali, basi ni bayana kuwa tamthilia teule ndio imefaidi kutokana na utenzi. Katika sura hii, tutajadili athari za mwingilianomatini katika udhamirishaji na mtindo wa *Kifo Kisimani*. Tutafafanua jinsi vipengele vya kimtindo vilivyotumika kimwingilianomatini ili kufanikisha dhamira ya ukombozi inayojitokeza katika *Kifo Kisimani*. Vipengele vya kimtindo vitakavyojadiliwa ni motifu ya tanzia na ya usaliti, uteuzi wa msamiati na matumizi ya jazanda. Aidha, tutaeleza jinsi tamthilia ya *Kifo Kisimani* ilivyofaidi kutokana na *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

## 4.2 Dhamira na Mwingilianomatini

Dhamira ni wazo kuu linalojitokeza katika kazi ya fasihi. Mwandishi anapoanza kuitunga kazi yake, huwa na ule ujumbe ambao angetaka kazi hiyo iwasilishe. Baadhi ya dhamira zinazoweza kujitokeza katika matini za kifasihi ni: ukombozi, ujenzi wa jamii adilifu, burudani, miongoni mwa mengine. Dhamira hukuzwa na mambo kadha ikiwemo maudhui, usawiri wa wahusika, mandhari na mtindo wa uwasilishaji wa ujumbe wenyewe. Dhamira ya *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* ni ukombozi.

*Utenzi wa Fumo Liyongo* ni mojawapo wa kazi za zamani za fasihi ya Kiswahili. Kwa hivyo, pana uwezekano kuwa Wa Mberia aliusoma utungo huu (ameandika makala kuhusu *Utenzi wa Fumo Liyongo* katika jarida la *Mulika*) na kuishia kuathiriwa kwa namna fulani katika mtindo na muundo wa *Kifo Kisimani*. Hili linathibitishwa na namna alivyomteua mhusika mkuu na sifa anazopewa, jinsi mhusika huyu anavyoendeleza dhamira ya ukombozi na vikwazo anavyopambana navyo katika harakati za ukombozi, muundo wa jamii yake, kifungo na hatimaye kuishia kusalitiwa na kakake. Sifa hii inadhihirika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* kwani Liyongo aliyapitia mengi ya yaliyopitiwa na Mwelusi. Anapangiwa kuuawa na utawala, anatiwa gerezani na hayimaye kuishia kuuawa na mwanawe wa kiume. Kwa msingi huu, tunaweza kuona kuwa *Kifo Kisimani* ina miangwi ya kidhamira ya *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

Jamii inayosawiriwa na utenzi huu ilikuwa kwenye matatizo. Walikuwa wakivamiwa na maadui wao wasipate wa kuwaokoa. Hivyo, walipompata Liyongo, wakahisi kuwa wamepata ngao yao.

*225. "Liyongo silaha yetu*
*kwa wut'e khasimu zetu*
*alikuwa ngao yetu."*
*wut'e wakinena haya.*

Maneno haya yanatuonyesha jinsi wanajamii walivyomuenzi Liyongo. Walimwona kama zawadi waliyotunukiwa nayo ili iwakomboe kutokana na matatizo yaliyowakumba.

Aidha, jamii inayosawiriwa na tamthilia ya *Kifo Kisimani* ilikuwa na matatizo mengi.

*Zigu:* *Ukivunja kanuni ya Butangi utateseka.*
*Andua:* *Tayari mateso ndiyo hewa wanayopumua Wanabutangi.*

(uk 91)

Mwelusi alikuwa tayari kuikomboa jamii yake kwa vyovyote vile kutokana na mateso haya. Anapofika nyumbani kutoka gerezani, mamake anamshauri atoroke kama hataomba msamaha kwa Bokono. Kwa ukakamavu, Mwelusi anakataa ushauri huu wa mamake.

*Mwelusi: La! Sitatoroka, mama. Butangi inahitaji wazalendo wake sasa hata kuliko nyakati za nyuma. Jana mlitangaziwa kwamba kumewekwa kanuni mpya. Kanuni inayozuia watu kuteka maji.... Mbali na mambo mengine, hii kanuni inahitaji kupingwa. Ni wajibu, mama. Kwa hivyo, leo tunakwenda kisimani kunywa maji... Huu utakuwa mwanzo wa kukiuka kanuni mbali mbali za kikatili. Huu utakuwa mwanzo wa mwisho...*

(uk 83)

Maneno haya ya Mwelusi yanatudhihirishia ari aliyokuwa nayo ya kuikomboa jamii yake. Anaendeleza dhamira ya ukombozi licha ya changamoto alizokumbana nazo katika harakati hizi. Ingawa alifariki baada ya kusalitiwa na kakake, ukombozi huu uliafikiwa kwani wale alikuwa amewazindua waliendeleza harakati hizi na kupata ukombozi uliolengwa na Mwelusi. Umati uliojitokeza, katika ikulu ya Butangi, kulipiza kifo cha Mwelusi ni ishara kuwa mhusika huyu alikuwa kipenzi cha wengi na kwamba walipenda juhudi zake za kuinasua jamii yake kutokana na minyororo ya udhalimu wa Bokono.

Kutokana na maelezo haya, ni bayana kuwa, kuna mwingilianomatini wa kidhamira na namna ya kukuza dhamira hii. Dhamira katika kazi zote mbili imekuzwa kwa usawiri wa maudhui yanayoshabihiana, uhusika unaolandana, mandhari yanayofanana na vilevile ploti za kazi hizi pia zinafanana kwa kiwango kikubwa.

## 4.3 Mwingilianomatini wa Kimtindo

Wamitila (2002:57) anasema kuwa, mtindo ni elementi ya kimsingi katika maana ya jumla ya kazi ya fasihi. Hii ni kwa sababu, mtindo huhusisha njia mbalimbali anazotumia mwandishi wa fasihi kuwasilisha ujumbe wake kwa wasomaji. Hivyo, tunapoangalia dhamira katika matini za kifasihi, hatuwezi kamwe kupuuza mtindo kwani ndio utakaotuelekeza kubainisha dhamira hiyo. Uchunguzi wa mtindo huhusisha mambo mengi. Katika sehemu hii, tutachunguza matumizi ya motifu ya tanzia, usaliti, uteuzi wa msamiati na vilevile jazanda.

### 4.3.1 Motifu ya Tanzia

Tanzia ni dhana inayorejelea kifo cha mhusika mkuu katika kazi ya fasihi. Kwa mujibu wa Wamitila (2003:219), ingawa dhana hii hutumiwa kurejelea utanzu mmoja wa tamthilia ambao unahusu kuanguka kwa nguli na kuishia kwa kifo, inaweza pia kutumika katika uhakiki kurejelea kazi yoyote ya kifasihi ambayo inaishia kwa anguko la mhusika mkuu. Katika *Utenzi wa Fumo*

*Liyongo* na *Kifo Kisimani*, kulitokea vifo vya wahusika wawili wakuu. Wahusika hawa ni Liyongo na Mwelusi katika mtiririko huo. Jamaa za wahusika hawa waliwasaliti kwa kusababisha vifo vyao. Ploti zote zinahusu maisha ya mashujaa hawa ambao walichukiwa na viongozi na hivyo, wakapangiwa kuuawa ili kuuzima kabisa upinzani wao. Motifu hii imetawala kazi zote mbili. Mfano, beti za kwanza 48 tu ndizo zinazoeleza asili na wasifu wa Liyongo ilhali beti zote zilizobakia (kutoka 49-230), zinahusu mpango wa kuuawa kwa Liyongo na hatimaye kifo chake. Hivyo, tunaweza kusema kuwa suala hili lilitawala kazi hii. Vilevile, mipango ya mauaji na hatimaye kifo cha Mwelusi, ilianza kutoka onyesho la pili hadi la kumi katika *Kifo Kisimani*. Hili linaonyesha kuwa suala hili pia lilitawala kazi hii.

Kifo kimetumika kuonyesha kuwa ukombozi hauji kwa urahisi. Lazima watu wengine wajitolee mhanga ili kuafikia lengo hili. Mfalme aliona kuwa Liyongo alikuwa na nafasi kubwa ya kuchukua uongozi, kwa vile alikuwa kipenzi cha wengi na umaarufu aliokuwa nao. Naye Mfalme alitaka kuendeleza uongozi wake wa kidkteta hivyo, akaamua kummaliza Liyongo ili azimio lake litimie. Kilichosababisha kifo cha Liyongo ni uzalendo wake kwa jamii yake pamoja na kuwa na sifa za kiongozi mwema. Alipofariki, kulikuwa na mwanzo mpya. Watu walionyesha kuzinduka. Walimtenga muuaji wa Liyongo hadi akafa kwa sababu ya tabu alizopitia. Hii ni ishara ya jamii inayoongozwa na maadili mema. Hawakuogopa Mfalme wala kumwonea huruma kijana huyu. Huu ulikuwa mwamko mpya kwa jamii hii. Hali kadhalika, kifo cha Mwelusi kilileta mwamko mpya kwa wanabutangi. Wanawake walioonekana kutengwa na uongozi walipata nguvu mpya. Kikosi kilichoelekea kwa Bokono na kumkamata pamoja na wafuasi wake kiliongozwa na mwanamke kwa jina Azena. Huu ni mwamko mpya kwani watu wawa hawa ndio waliokuwa wamejinyamazia walipokuwa wakinyanyaswa. Hivyo, tunaweza kusema kuwa, kifo cha Mwelusi kilileta mwamko mpya kwa Wanabutangi. Mwamko mpya katika muktadha huu, ni ukombozi ambao ndio dhamira kuu ya *Kifo Kisimani*.

Kifo kinachotokea kisimani kina ishara ya mwanzo wa maisha mapya. Kisima ni chemchemi za maji ambayo ni muhimu sana kwa uhai wa viumbe mbalimbali. Hivyo, kifo kilipotokea kisimani kiliibua maana ya kifo cha uongozi mbaya na kuzaliwa kwa uongozi mpya wenye matumaini kwa wote. Huu ndio ukombozi uliolengwa na Kijumwa na Wa Mberia. Kwa sababu hii,

tunaweza kusema kuwa, motifu ya tanzia imetumika kukuza na kuiweka wazi dhamira ya *Kifo Kisimani* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

### 4.3.2 Motifu ya Usaliti

Katika harakati za ukombozi, Liyongo na Mwelusi walikinzana na viongozi wa jamii zao. Hili liliwafanya viongozi hawa kuchukua hatua ya kuwaua ili upinzani wao uishe. Mitego waliyowekewa wahusika hawa haikufaulu hivyo wazo la kutumia jamaa zao likaafikiwa na tawala za jamii zote mbili. Mwana wa Liyongo alitumika kumuua babake naye Gege akatumika kumuua Mwelusi. Vijana hawa waliwasaliti wapendwa wao kwani walihitajika kuwalinda kutokana na maovu waliyokuwa wakitendewa na viongozi. Badala ya kufanya hivi, waliwaua ili kutimiza tamaa zao.

Motifu hii imetumika kimwingilianomatini kwani vitendo vya usaliti katika kazi zote mbili vinafanana. Tunaposoma kisa cha Gege katika *Kifo Kisimani*, kinatokea kama mwangwi wa kisa cha mwana wa Liyongo katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Motifu hii inatumika kuonyesha changamoto zinazowakumba wanaharakati wa ukombozi. Hali kadhalika, inatudhihirishia jinsi wanajamii walivyotokwa na maadili kwa sababu ya tamaa ya mali na umaarufu. Licha ya kuwa Liyongo na Mwelusi hawakuwa na hatia yoyote, jamaa zao waliwaua ili wapate maisha mazuri waliyoahidiwa na viongozi. Hali kadhalika, inaonyesha jinsi vijana wanavyotumika na viongozi kutekeleza maovu yao, hasa kwa kukabiliana na wapinzani wa kisiasa.

### 4.3.3 Uteuzi wa Msamiati

Kijumwa, ambaye ni mzaliwa wa Pwani amekita kazi yake katika mazingira ya Pwani. Kwa mfano, matendo makuu yalifanyika mjini Pate na mfalme ndiye alikuwa akiwaongoza. Maneno kama vile sultani - mtu mwenye cheo cha utawala wa kifalme, ni neno linalotumika sana sana kwenye maeneo ya pwani kwa sababu ya athari za kiarabu. Pia, mwandishi huyu ametumia lahaja ya Kiamu kuandika utenzi huu. Kwa mfano:

*70. Sulutwani kabaini*
*"Hela kamzoezeni*
*mumrejeze muini*
*nimeomba nami haya."*

*71.  "Mwambieni, 'Tusafiri*
*hata Pate tukajiri*
*hapana tena khatari*
*habari tumesikiya*

*117. Wakiinuka kuteza*
*Liyongo akatokeza*
*khaufu zaliwakaza*
*mbio zikawapoteya*

*118. Kwa wut'e wakakimbiya*
*hapana alosaliya*
*Liyongo kaitokeya*
*mabarani karejeya*

Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya maneno ya lahaja ya Kiamu iliyotumika katika utenzi, kama inavyoonyeshwa kwenye beti zilizonukuliwa halo juu:

muini kwa maana ya mjini

kuteza kwa maana ya kucheza

kaitokeya likimaanisha kajitokea

wut'e likimaanisha wote

Kwa upande mwingine, athari za mwingilianomatini zinajitokeza katika uteuzi wa maneno katika *Kifo Kisimani*. Licha ya kuwa Wa Mberia ni mzaliwa wa bara, hasa upande wa mashariki mwa Kenya, ametumia msamiati unaoashiria mazingira ya Pwani. Kwa mfano, kisima kilichozua mzozo tamthiliani kinajulikana kama Kisima cha Mkomani. Neno hili linaashiria dhana kuwa, mahali palipokuwa na kisima hiki palikuwa na mti wa mkoma. Jamii nyingi za kiafrika, ikiwemo jamii ya Waswahili inayopatikana Pwani ya Afrika Mashariki, zina mazoea ya kukipa kitu au

mahali majina kulingana na ishara inayolinganishwa na eneo au kitu hicho. Ishara hizi zinaweza kuwa; mti mkubwa, mto au hata mlima. Sababu hii ndiyo iliyotufanya kuamini kuwa kulikuwa na mkoma karibu na kisima hiki ndiposa kikapewa jina hili. Mkoma ni mti wa jamii ya mnazi uotao kwenye sehemu kame ya ardhi. Mnazi ni mti maarufu sana eneo la Pwani, kwa hivyo, hata mkoma, kwa vile ni wa jamii moja na mnazi, basi kuna uwezekano mkubwa kuwa hupatikana eneo hili pia. Wengi wa wenyeji walikitegemea sana kisima hiki kukata kiu chao cha kila siku. Kwa sababu hii, tunaweza kusema kuwa, tamthilia hii imekitwa katika mazingira yanayoshabiana na yale ya *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

Aidha, matumizi ya neno 'Mtemi' kurejelea kiongozi wa nchi pia lilitumika kimwingilianomatini. Mtemi ni neno lenye maana ya kiongozi mwenye hadhi sawa na mfalme. Neno hili pia linadhihirisha mshabaha wa kimazingira baina ya *Kifo Kisimani* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Hii ni athari ya mwingilianomatini katika tamthilia hii kwa vile haikuwa lazima mwandishi huyu kutumia maneno yanayoashiria mazingira ya aina hii. Hata hivyo, huenda athari hizi ndizo zilizomwongoza kuyatumia mazingira haya.

Isitoshe, miongoni mwa ngoma ambazo zingechezwa katika mkutano wa hotuba ya Mtemi Bokono ni Chakacha. Hii ni ngoma maarufu miongoni mwa jamii ya Pwani. Ngoma hii huambatana na nyimbo zenye mahadhi ya Taarab na huchezwa na wanawake katika Pwani ya Afrika Mashariki. Pia katika matukio yanayotiririka akilini mwa Mweke anapopanga jinsi atamhadaa Gege ili akubali kumuua nduguye, tunaona msamiati wa Pwani ukirejelewa. Kwenye matukio haya, Mweke wanazungumza na Talui wakijaribu kufikiria jinsi watu watakavyokuwa wakizungumza baada ya harusi ya Gege na Alida.

> *Mweke: .... Akilini mwangu tayari ninayaona mazungumzo ya watu baada ya arusi. Nawaona wavuvi wawili ufuoni wakizungumza [Anajifanya mvuvi mmojawapo. Anachukua pondo na kuanza kuitumia ili kusukuma dau karibu na ufuo]. Hujambo Bate!*
>
> *Talui: [Ambaye amechutama 'ili kuyakumba maji kutoka dau lake'] Sijambo Mile. Salama?*
> *Mweke: Salama! Watu nyumbani wazima?*
> *Talui: Wote wazima. Ulisafiri au nini? Sijakuona baharini kwa muda mrefu?*
>
> ( Uk 70)

Kupitia mazungumzo haya, msamiati uliotumika unadhihirisha wazi kuwa tamthilia hii imekitwa katika mazingira ya Pwani ambako kuna bahari na shughuli za uvuvi. Aidha, Wa Mberia ametumia msamiati wa Kiswahili sanifu katika kazi nzima. Hakuna mahali alipochanganya au kuhamisha ndimi.

Maelezo tuliyoyatoa hapo juu yanadhihirisha wazi athari za mwingilianomatini katika tamthilia teule. Mwandishi ametumia msamiati unaohusiana na mazingira ya Pwani, licha ya kuwa angetumia mazingira ya eneo alikozaliwa au mandhari nyingine ya kubuni. Hata hivyo, kuna uwezekano kuwa, athari za mwingilianomatini kutoka kwa *Utenzi wa Fumo Liyongo*, zilichangia katika uteuzi wa mazingira haya ya Pwani ili kutumika kwenye tamthilia ya *Kifo Kisimani*.

### 4.3.4 Matumizi ya Jazanda

Jazanda ni mbinu inayohusishwa na matumizi ya picha. Hizi ni zile picha ambazo humjia msomaji wa kazi ya fasihi. *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* zimesawiri jazanda mbalimbali. Jazanda hizi zimetumika kukuza dhamira na vilevile, zimedhihirisha mwingilianomatini baina ya kazi hizi.

Utenzi teule umeanza kwa kutueleza wasifu wa Liyongo. Katika ubeti wa 7, tunaambiwa kuwa Liyongo alikuwa mpana na mrefu sana. Beti za 13-15 zinamweleza kama mwanamume mkakamavu na aliyekuwa na nguvu kama simba. Hakuogopa kutembea usiku wala mchana kwani kwake, haya yote yalikuwa mamoja. Mtu huyu angekutokea ghafla, ungejawa na hofu kiasi cha kujiendea haja ndogo. Zaidi ya hayo, angekukodolea macho, ungezimia kwa hofu ambayo ingekuingia. Maelezo haya yanatuchorea picha ya mhusika huyu akilini ingawa hatujakutana naye ana kwa ana. Anaonekana mtu mwenye nguvu na umbo la kuogofya. Picha hii inamsawiri kama mwanamume wa vita na ushujaa wake unajitokeza wazi. Ushujaa huu unatuelekeza kuamini kuwa alikuwa na uwezo wa kuiletea jamii yake ukombozi iliyouhitaji.

*Kifo Kisimani* pia imesawiri jazanda inayoshabihiana na ile tuliyojadili katika utenzi teule. Tamthilia imeanza kwa kutupa wasifu wa Mwelusi kuwa ni kijana wa kiume wa miaka 24 hivi. Hivyo, picha ya mhusika huyu inamjia msomaji. Kwa kawaida, katika umri huu, mtu huwa na nguvu na kwa vile hakuwa na majukumu mengi (mfano, hakuwa ameoa), tunaamini kuwa alikuwa na nafasi bora ya kuipigania jamii yake kama alivyokuwa Liyongo.

Taswira nyingine ni pale ambapo Liyongo alikuwa gerezani, na jinsi askari walivyokuwa wakila chakula alichokuwa akiletewa kisimfikie chakula chochote. Vilevile, taswira ya jinsi alivyoikereza minyororo na hatimaye kuwa huru inajichora akilini mwa msomaji wa kazi hii. Aidha, taswira ya gerezani inajitokeza pia katika *Kifo Kisimani*. Tunaelezwa jinsi askari walivyokuwa wakila chakula alicholetewa Mwelusi. Jazanda hii inatupa sifa za wahusika hawa kuwa ni walafi. Hali kadhalika, taswira ya jinsi Mwelusi alivyopata tupa ya kuikata minyororo yake na kujipatia uhuru. Taswira hii inatuelekeza kuelewa kuwa binadamu anaweza kuyatatua matatizo yake kwa njia mbalimbali hivyo, hapaswi kukata tamaa kamwe. Aidha, inaonyesha changamoto za ukombozi; mambo ambayo watu wanaofuatilia ukombozi huweza kuyapitia.

Kuna pia taswira ya jinsi harusi kati ya mwana wa Liyongo na bintiye Mfalme ingekuwa. Tunaambiwa kuwa wangeshona nguo nzuri za bwana na bibi harusi. Wangecheza ngoma na kufurahia harusi hiyo. Aidha, harusi ya Gege na Alida inatujia akilini tunaposoma maelezo yaliyotolewa na Mweke na Talui katika tamthilia teule. Kulingana nao, harusi hii ingefana sana. Bwana na bibi harusi wangepambwa kwelikweli. Aidha, harusi hii ingekuwa mazungumzo ya mtaani kwa vile watu hawakuwa wamewahi kushuhudia harusi kama hiyo hapo awali. Maelezo haya yanatuelekeza kuelewa harusi ya kifahari waliyoahidiwa vijana hawa.  Kwa hivyo, harusi hizi zote zingekuwa za kufana sana. Jazanda hii inatuonyesha mbinu za uongo zinazotumiwa na viongozi wanapotaka kuafikia malengo yao maovu. Wandishi wanakusudia kutahadharisha jamii dhidi ya hadaa za viongozi na kuwashauri kufikiria sana kabla ya kufanya mambo ambayo matokeo yake yanakuwa na madhara makubwa.

Jazanda ya kifo cha Liyongo mle kisimani ni kilele cha kazi nzima. Liyongo alikuwa mhusika mkuu katika kazi hii na kifo chake kinaashiria mwisho wa hadithi. Mhusika huyu alifariki akiwa amejihami tayari kukabiliana na adui wake. Hali yake mle kisimani iliwatishia wengi. Waliogopa kwenda kisimani wakidhani kuwa angewashambulia. Mwandishi anataka kusisitiza kuwa mtu hapaswi kukata tamaa, anapokuwa katika harakati za ukombozi, mpaka dakika za mwisho. Watu walisikitishwa na kifo cha shujaa wao na kama njia ya kumpa heshima, wakamtenga muuaji wake. Hawakutaka kuhusishwa naye kwa njia yoyote ile. Kijana alipatwa na tabu, akajifia pia lakini chake, kilikuwa kifo cha aibu.

Vilevile, kifo cha Mwelusi kwenye Kisima cha Mkomani ni kilele cha tamthilia ya *Kifo Kisimani*. Kijana huyu anafariki akiwa kwenye harakati za kuleta ukombozi kwa jamii yake. Kama tulivyoona katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, kifo kwenye hiki kisima kiliashiria mwisho wa maisha mabaya chini ya uongozi wa Bokono, na mwanzo wa maisha mapya kwa Wanabutangi. Baada ya kifo cha Mwelusi, wananchi waliokuwa na ghadhabu walivamia Bokono na Wafuasi wake, wakawafunga na kuwatia gerezani. Nguvu za Bokono zikawa hazifanyi kazi tena. Alikuwa chini ya nguvu nyingine; nguvu za wananchi. Hii ni ishara ya kuonyesha kuwa ukombozi hauji kwa urahisi. Ilimgharimu Mwelusi maisha yake ili Butangi ipate ukombozi. Hivyo, taswira hii imetumika kukuza na kuiweka wazi dhamira ya mwandishi wa tamthilia ya *Kifo Kisimani*.

**4.3.5 Tathmini**

Kama tulivyotangulia kusema, tamthilia ya *Kifo Kisimani* imefaidi kutoka kwa *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Tamthilia hii ina dhamira ya ukombozi kama ilivyo katika utenzi husika. Katika kukuza dhamira hii, Wa Mberia amewasawiri wahusika wanaolandana na wale wa *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Vilevile, mandhari yanalandana katika kazi zote mbili. Haya, yashashughulikiwa katika sura ta tatu.

Isitoshe, Wa Mberia ametumia mbinu za kimtindo zinazoshabihiana na zile zilizotumiwa na Kijumwa. Tumeona kuwa alitumia motifu ya tanzia na usaliti kudhihirisha kuwa, ukombozi hauji kwa urahisi. Vilevile, kifo kilichotokea kisimani kinaashiria mwanzo wa maisha mapya. Kifo kina maana ya mwisho wa maisha ya kiumbe fulani. Kisima ni chemchemi ya maji ambayo ni muhimu sana kwa uhai wa viumbe vyenye uhai. Hivyo, kifo cha Mwelusi kiliashiria mwisho wa maisha ya udhalimu wa Bokono na mwanzo wa maisha mapya yaliyowanufaisha wanajamii wote kwa jumla. Wananchi waliozinduliwa na Mwelusi waliendeleza harakati za ukombozi hata baada ya kifo chake. Hata ingawa kwenye utenzi teule hakukuwa na aina hii ya uzindushi, sehemu hii ya tamthilia imejitokeza kama uboresho wa utenzi kutegemea mpito wa wakati. Hii ni kwa sababu, tamthilia teule iliandikwa enzi ambazo viongozi wanateuliwa na wananchi na kuwaondoa mamlakani wanapotaka, hivyo ilikuwa rahisi kwa Wanabutangi kumwondoa Bokono mamlakani waliposhirikiana. Tunasema sehemu huu inajitokeza kama uboresho wa utenzi teule kwa vile, enzi za uandishi wa utenzi huu, uongozi ulikuwa chini ya ufalme na wananchi

hawakuwa na uhuru wa kujichagulia kiongozi wao kwa vile ulikuwa wa kurithi kutoka kwa familia.

Hali kadhalika, tamthilia hii imefaidi kutika uteuzi wa msamiati. Kuna msamiati uliodhihirisha mazingira ya Pwani. Pia, mwandishi wa tamthilia hii ametumia Kiswahili sanifu. Hakuna pahali alipochanganya ndimi. Kama tulivyosema hapo awali, huyu ni mzaliwa wa bara na hasa upande wa mashariki mwa Kenya. Lakini, ametumia msamiati wa uswahilini kama inavyothibitishwa na maelezo tuliyoyatoa hapo awali katika sura hii. Hii ni athari ya mwingilianomatini katika kiwango hiki cha mtindo.

Jazanda pia ni kipengele cha mtindo kilichojitokeza kudhihirisha mwingilianomatini katika kazi hizi. *Kifo Kisimani* imeonekana kutumia jazanda zinazolandana na zile za *Utenzi wa Fumo Liyongo* katika kukuza dhamira ya ukombozi katika kazi zote mbili. Jazanda tulizozijadili katika tamthilia teule, zinanuia kumkuza mhusika mkuu (Mwelusi) na wakati huo huo zikiikuza dhamira ya mwandishi. Hivyo, ni bayana kuwa, *Kifo Kisimani* ilifaidi kutoka kwa *Utenzi wa Fumo Liyongo* katika kipengele hiki cha kimtindo.

**Hitimisho**

Katika sura hii, tumejadili dhamira na vipengele teule vya kimtindo. Tumeonyesha jinsi vipengele hivi vinavyodhihirisha mwingilianomatini katika kazi zinazohusika katika utafiti huu. Aidha, tumeonyesha kuwa, *Kifo Kisimani* ilifaidi kutoka kwa *Utenzi wa Fumo Liyongo* katika ukuzaji wa dhamira. Dhamira ya tamthilia hii ni ukombozi, kama ilivyo katika utenzi husika. Tumebaini kuwa, Wa Mberia amesawiri wahusika wake kwa njia iliyo sawa na ile iliyotumiwa na Kijumwa. Vilevile, ametumia motifu ya tanzia na ile ya usaliti kuonyesha hatima ya wapinzani katika utawala wa kidkteta. Motifu hizi pia zilijitokeza katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, hivyo tamthilia teule ilifaidi kutokana na utenzi huu katika kiwango hiki cha kimtindo. Hali kadhalika, matumizi ya jazanda katika kazi zote yameonyesha mshabaha. Jazanda hizi vilevile zimeikuza na kuiweka wazi dhamira ya ukombozi katika kazi zote mbili. Vilevile, athari za mwingilianomatini zimejitokeza katika uteuzi wa msamiati. Baadhi wa msamiati katika *Kifo Kisimani* umeonyesha mshabaha na ule wa utenzi husika. Hili limetubainishia miktadha mbalimbali ambayo matukio ya kazi hii yalitokea. Kutokana na maelezo haya, ni bayana kuwa, kuna athari za mwingilianomatini katika udhamirishaji na mtindo wa *Kifo Kisimani*. Hatua hii

imetuwezesha kuafikia lengo letu la tatu ambalo lilikuwa ni kubainisha athari za mwingilianomatini katika udhamirishaji na mtindo wa tamthilia ya *Kifo Kisimani*. Aidha, swali letu la tatu kuwa, kuna athari za mwingilianomatini katika udhamirishaji na mtindo wa tamthilia ya *Kifo Kisimani* limeweza kujibiwa.

# SURA YA TANO

# MATOKEO YA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii, tutatoa muhtasari matokeo ya utafiti huu na jinsi tulivyoweza kuafikia malengo ya utafiti. Vilevile, tutatoa mapendekezo kwa watafiti wa baadaye kuhusiana na mada yetu ya utafiti. Hatimaye, tutatoa marejeleo ya kazi tulizozitumia kufanikisha utafiti wetu.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulikusudia kuchunguza mwingilianomatini kati ya *Utenzi wa Fumo Liyongo* na tamthilia ya *Kifo Kisimani*. Tuliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini ambayo husisitiza kuwa, matini huakisiana kwa kiwango fulani na matini za awali zinazohusiana nayo. Aidha, matini haijitegemei kimaana, maana yake hubainika baada ya kuhusishwa na matini nyingine ya awali. Sababu ni kuwa, mwandishi huweza kuchota malighafi yake kutoka kwa kazi za awali. Baadhi ya mambo yanayoweza kuigwa kutoka kwa kazi tangulizi ni maudhui, dhamira, ploti, usawiri wa wahusika, namna ya usimulizi, vishazi na hata sentensi. Ni kwa misingi hii ambapo tulichagua kazi mbili ambazo ni *Utenzi wa Fumo Liyongo* na tamthilia ya *Kifo Kisimani* na kuzihusisha na utafiti huu ili kuzihakiki kwa msingi huu wa kinadharia.

Kutokana na utafiti huu, tumebainisha kuwa kuna vipengele vya mwingilianomatini katika utenzi na tamthilia husika. Vipengele vilivyojitokeza katika kazi hizi ni: maudhui, dhamira, uhusika, mandhari, usimulizi, msuko na vilevile mbinu ya mhusianisho. Mhusianisho hutokea pale, mtu anapoisoma kazi fulani ya fasihi, kazi hii inamfanya kuikumbuka kazi nyingine ya awali inayohusiana nayo. Kwa mfano, tunaposoma kuhusu wasifu wa Mwelusi katika *Kifo Kisimani*, inatuelekeza kumhusisha na Liyongo katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Vipengele hivi vya mwingilianomatini vimeonyesha mfanano katika kazi husika. Uchunguzi huu ulituwezesha kuafikia lengo letu la kwanza la utafiti huu. Aidha, swali la utafiti la kwanza pia limeweza kujibiwa kwani tumeweza kubainisha vipengele vya mwingilianomatini vinavyojitokeza katika kazi husika.

Aidha, tulichunguza jinsi *Kifo Kisimani* na *Utenzi wa Fumo Liyongo* zinavyoingiliana katika viwango vya kimaudhui, dhamira, uhusika, mandhari na usimulizi. Kutokana na utafiti huu, tumebainisha kuwa kazi hizi mbili zina dhamira ya ukombozi. Ili kukuza dhamira hii

kimwingilianomatini, maudhui katika kazi zote mbili, yalisawiriwa kwa namna inayoshabihiana. Kwa mfano, Mfalme na Bokono hawakuzingatia maadili mema katika uongozi wao. Tamaa ya uongozi iliwafanya kutekeleza maovu katika jamii zao. Waliwaua wapinzani wao ili kujihakikishia kipindi kirefu cha uongozi. Mauaji ya Liyongo na Mwelusi yanatekelezwa na jamaa zao. Jambo hili linaendeleza maudhui ya usaliti. Hali kadhalika, viongozi hawa walitumia rasilimali za umma kwa manufaa yao wenyewe. Walitumia askari kujidumisha mamlakani. Uongozi wao mbaya ulisababisha utabaka ambapo tunapata jamii zao zikiwa na matabaka mawili makuu; lile la wasionacho na lile la walionacho. Kundi la walionacho lilikuwa la watu wachache waliokuwa katika utawala na lile la wasionacho lilikuwa la watu wengi ambao walikuwa watawaliwa. Kulingana na maelezo haya, ni bayana kuwa Wa Mberia alifanikiwa kusawiri maudhui kimwingilianomatini. Kadhalika, jambo hili linadhihirisha kuwa, binadamu huathiriwa na masuala takribani yaliyo sawa. Hivyo, tunaona kuwa, mambo yaliyoiathiri jamii ya *Utenzi wa Fumo Liyongo*, yanaiathiri jamii ya Ki*fo Kisimani* takribani karne moja baadaye.

Vilevile, mwingilianomatini umejitokeza kutokana na usawiri wa wahusika. Mama alipewa jukumu la kumlea shujaa katika kazi zote mbili. Hili linadhibitishwa na ukweli kuwa, wazazi wa kiume hawakupewa nafasi yoyote katika ploti za kazi hizi husika. Mwelusi, katika *Kifo Kisimani*, alisawiriwa kama Liyongo wa *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Wahusika hawa walikinzana na viongozi wa jamii zao. Suala hili linawafanya wakamatwe na kutiwa gerezani. Ingawa wanafaulu kutoroka kwa njia sawa, wanaishia kusalitiwa na jamaa zao. Hali kadhalika, tunaposoma kuhusu matendo ya Gege, yanatuelekeza kumhusisha na mwana wa Liyongo kwani vijana hawa walitekeleza majukumu yaliyoshabihiana katika kazi zote mbili. Gege alihadaiwa akamuua kakake naye mwana wa Liyongo alidanganywa akamuua babake, Liyongo. Kutokana na maelezo haya, ni dhahiri kuwa, *Kifo Kisimani* ilifaidi kutokana na utenzi husika kwani Wa Mberia ameonekana kuwa alichota masuala ya uhusika katika kazi tangulizi ambayo in *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

Hali kadhalika, mandhari ni kipengele kingine ambacho kimeonyesha sifa ya mwingilianomatini katika *Kifo Kisimani* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Mandhari tuliyochunguza ni ile ya kijiografia ambayo ilihusisha mandhari ya ikulu, gereza, na pia kisimani. Hapa, tulibainisha kuwa, mandhari huathiri matendo na maneno ya wahusika katika kazi za fasihi. Mandhari ya gereza iliandamana

na mateso kwa wafungwa. Askari ndio waliohusishwa na mateso haya kwa watu waliostahili kuwalinda. Aidha, ikulu inahusishwa na uongozi na viongozi katika kazi zote mbili walitumia nafasi zao vibaya. Maamuzi yaliyofanyiwa ikuluni hayakuwa ya kuzijenga jamii zao bali yalikuwa ya kuwahakikishia viongozi uongozi mrefu. Vilevile, mandhari ya kiwakati imetumika kudhihirisha sifa ya mwingilianomatini na vilevile kukuza maudhui na dhamira ya kazi husika.

Isitoshe, sifa ya mwingilianomatini imedhihirika katika kiwango cha usimulizi. Hii ni kwa sababu, *Kifo Kisimani* imeonekana kuuakisi *Utenzi wa Fumo Liyongo* katika kiwango hiki cha usimulizi. Kutokana na utafiti wetu, ploti za kazi zote mbili zimeonyesha mshabaha. Hili linawezeshwa na hali kwamba, wahusika katika kazi hizi walisawiriwa kwa njia zinazoonyesha mkuruba. Hivyo, matendo yao yameonyesha kuendeleza ploti zinazoshabihiana. Vilevile, matumizi ya nyimbo na ngoma katika kazi zote mbili yamedhihirisha mwingilianomatini kwani vipengele hivi vya fasihi simulizi vilitumiwa kutekeleza kazi sawa katika kazi husika. Vipengele hivi vilitumika kutekeleza kazi ya kuburudisha wanajamii.

Uchanganuzi wa vipengele hivi umetuelekeza kubaini kuwa, *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* zimeingiliana kimatini katika viwango vya vipengele hivi. Aidha, ni bayana kuwa Wa Mberia ameiga mambo fulani kutoka kwa utenzi husika. Sababu ni kwamba, utenzi huu ndio kazi tangulizi. Kwa sababu hii, mambo yanayoonyesha mkuruba katika *Kifo Kisimani* yalitumika kiurejelezi na hivyo, tunaweza kuyahusisha na yale ya utenzi husika. Uchunguzi huu umetuwezesha kuafikia lengo letu la pili na pia kujibu swali la pili la utafiti kwani tumeweza kuonyesha viwango vya kimaudhui na kifani vinavyodhihirisha sifa ya mwingilianomatini katika kazi husika.

Hatimaye, tumehakiki athari za mwingilianomatini katika udhamirishaji na mtindo wa tamthilia ya *Kifo Kisimani*. Hapa, imebainika kuwa mtindo wa kazi fulani ya kifasihi ndio hutuelekeza kubainisha dhamira ya kazi hiyo. Hivyo, tunapoangalia dhamira katika matini za kifasihi, hatuwezi kupuuza mtindo. Vipengele vya kimtindo tulivyovichunguza vimeonyesha kudhihirisha sifa ya mwingilianomatini kwani vimetumika kukuza dhamira katika kazi zote mbili. *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* zina dhamira ya ukombozi. Matendo na maneno ya wahusika katika kazi zote mbili yameonyesha kukuza dhamira hii. Kwa sababu hii, tunaweza kusema kuwa, *Kifo Kisimani* inauakisi utenzi, tukizingatia jinsi mwandishi wa tamthilia hii

alivyowasawiri wahusika wake katika mandhari inayoshabihiana na ile ya utenzi husika. Usawiri huu ulitumika kukuza maudhui na vilevile dhamira ya ukombozi. Athari za mwingilianomatini zilijitokeza kutokana na jinsi Wa Mberia alivyotumia motifu ya tanzia na ile ya usaliti. Pia, msamiati alioutumia katika tamthilia hii unadhihirisha mkuruba na ule wa *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Hali kadhalika, jazanda zilizojitokeza katika tamthilia hii zilishabihiana na zile za utenzi husika. Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa, kuna athari za mwingilianomatini katika udhamirishaji na mtindo wa *Kifo Kisimani*. Kwa kufanya hivi, tumeafikia lengo letu la tatu na pia tumeweza kujibu swali letu la tatu katika maswali yaliyotuongoza katika utafiti wetu.

Hata hivyo, ni bora ieleweke kuwa, utafiti huu umebaini kuwa, uhusiano baina ya *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Kifo Kisimani* ni ule wa kimwingilianomatini na wala sio utohozi. Utohozi wa fasihi ni kule kuchukua kazi iliyoko katika utanzu mmoja na kuiwasilisha katika utanzu mwingine. Kwa mfano, kuweka riwaya katika muundo wa filamu. Kwa upande mwingine, mwingilianomatini huhusisha urejelezi wa vipengele fulani katika kazi ya awali ili kuiunda kazi mpya. Kwa sababu hii, hatuwezi kusema kuwa mwandishi wa *Kifo Kisimani* ni kimelea kwani kuna vipengele ambavyo vinatofautisha kazi hizi mbili ingawa utafiti huu haukujihusisha na kuvibainisha. Hivyo, vipengele vilivyodhihirisha sifa ya mwingilianomatini katika kazi zetu teule, vimetumika kiurejelezi ili kufanikisha maana ya tamthilia husika.

**Hitimisho**

Nadharia ya mwingilianomatini inashikilia kuwa, matini za kifasihi hazijitegemei kimaana bila kuhusishwa na matini nyingine ya awali. Sababu ni kuwa, mwandishi hujihusisha na kukusanya na kupanga yaliyokuwemo hapo awali ili kuunda matini yake. Hivyo, matini atakayoiunda mwandishi huyu, huwa ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingi tangulizi. Baadhi ya mambo ambayo mwandishi anaweza kuyachota kutoka kwa kazi ya awali ni ploti, maudhui, msamiati, usimulizi miongoni mwa mengine. Kwa sababu hii, matini za kifasihi huweza kuakisiana kwa kiwango fulani. Msingi huu wa kinadharia umetuwezesha kubainisha kuwa, Wa Mberia alichota na kuiga mambo fulani kutoka kwa kazi tangulizi ambayo ni *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Kauli hii inathibitishwa na ukweli kwamba, kuna vipengele vinavyoonyesha sifa ya mwingilianomatini baina ya kazi hizi mbili. Aidha, uelewekaji wa tamthilia hii unaweza kufanikishwa kwa kuihusisha na utenzi husika. Hivyo, ni bayana kuwa, tamthilia hii ilifaidi

kutokana na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa, kuna mwingilianomatini kati ya *Utenzi wa Fumo Liyongo* na tamthilia ya *Kifo Kisimani*, na mwingiliano huu unachangia katika maana ya tamthilia husika.

**Mapendekezo**

Utafiti huu ulichunguza mwingilianomatini baina ya kazi za tanzu tofauti za kifasihi. Tulikusudia kudhihirisha kuwa, mwingilianomatini hautokei tu katika kazi za utanzu mmoja kama ilivyoonekana kudokezwa na tafiti za awali. Kuna haja ya watafiti wa baadaye kukuza dhana hii kwa kuendeleza uchunguzi zaidi kuhusu mwingilianomatini baina ya kazi za tanzu tofauti, hasa wakihusisha vipengele ambavyo hatukuweza kuvishughulikia katika utafiti huu. Miongoni mwa kazi zinazoweza kufanikisha utafiti wa aina hii ni riwaya ya *Usiku Utakapokwisha* - M. Msokile na tamthilia ya *Giza Limeingia* - E. Mbogo.

# MAREJELEO


Allen, G. (2000). *Intertextuality*. London: Routledge.

Bakhtin, M. (1981). *The Dialogic Imagination. Four Essay.* Austin: University of Texas.

Bosibori, B T. (2016). "Mwingiliano Matini Kati ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya*". Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Diegner, L. (2005). "Intertextuality in the Contemporary Swahili Novel. Euphrase Kezilahabi's *Nagona* and William E. Mkufya's *Ziraili na Zirani."* Katika *Swahili Forum* vol 22:25-35.

Gathara, F.K (2015). "Taswira ya Jagina katika Tendi: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Nabii Isa". Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Holy Bible, (2001). *King James Easy Reading Edition*. Good Year: G.E.M: Publishing

Kea, P. (2016). *Kigogo*. Nairobi: Story Moja Publications.

Khatib, M.S (1985). "Utenzi wa Mwanakupona" katika *Mulika* No. 17. Dar es Salaam: TUKI

King'ei, G. K. (2001). "Historical and Folkloric Elements in Fumo Liyongo's Epic." *Folklore*. ISSN 1406-0957 (2001):78-86

Kipyegon, K. E. (2013). "Nafasi na Utambulisho wa Mwanamke katika Natala na Kifo Kisimani." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Matei, K.A. (2017). *Chozi la Heri*. Nairobi: One Planet Publishing Media Services Limited.

Muhammad, K. (1913). *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House Ltd.

Ngesa, K.A na wengine. (2015). *"*Mwingilianomatini Katika Tamthilia za Kiswahili: *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo*". *Swahili Forum* 22:42-71

Njogu, K na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njoroge, H.G. (2007). "Mwingilianomatini katika Fasihi ya Kiswahili. Tata za Asumini na Rosa Mistika". Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Ochoki, J.M (2005). "Sitiari, Jazanda na Mwingiliano Matini katika Nagona na Mzingile". Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Raj, P.P.E. "Text/Texts: Interrogating Julia Kristeva's Concept of Intertextuality". *Research Journal of Humanities and Social Sciences* 2319-7889(3) (2015):77-80

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

__________ (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd

__________ (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Wa Mberia, K. (1989). “Fumo Liyongo" katika *Mulika* No. 21. uk 25-43. Dar es Salaam: TUKI

____________ (2001). *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba Publishers.

Waweru, G. N. "Usimulizi katika Tamthlia za Kithaka wa Mberia." *Swahili Forum*. 23(2016): 47-63